Kitendawili

Bwana awabariki. Hakika naona kuwa ni majaliwa ma—makuu kuwa hapa asubuhi ya leo. Nilikuwa. . .Ni baraka isiyotarajiwa, kwa sababu mimi, kuwazia kwamba ningekuwa na majaliwa haya kupata kuzungumza zaidi sana nanyi hasa, kile tungewazia, tungekiita, "kundi teule," wahudumu na ndugu zangu hapa wanaoshirikiana katika mkutano huu na kuufanikisha. Nilitamani fursa hii. Kwa njia hii, ninapata nafasi wakati mwingine kueleza mambo ambayo si—ambayo siyaelezei jukwaani, maana mko kwenye kusanyiko lililochanganyikana kule.

2 Nami nilikutana na wakili hapa asubuhi ya leo, mmoja wa ndugu, Wafanya Biashara Wakristo. Na jana usiku nilikuwa nikizungumza juu ya Zakayo. Mara akiwa pale, mwajua, wakati aliponinii. . .Yesu alikuwa katika. . .Ilikuwa ni vigumu kwake kuamini; kama vile ule mchezo mdogo wa kuigiza ulivyokuwa, kwamba, "Hakuwa nabii." Lakini wakati Yesu aliposimama chini ya ule mti, akatazama juu na kumwita jina, na akashuka. Kamwe sikuwasimulia yaliyompata Zakayo. Mwajua kilichompata jamaa huyo? Alifanyika mwanachama wa Wafanya Biashara wa full Gospel, na mwanachama mwanzilishi pale, ni kweli. Bila shaka, Yesu asingekuwa na chochote kile ila full Gospel, mwajua. Kwa hiyo, yeye akiwa ni mfanya biashara, hiyo ilikuwa ni sehemu ya ninii yenu. . .Kwa hiyo, mngeweza kukumbuka jambo hilo, basi.

3 Na kwa hiyo ni—nilikuwa nikizungumza hivi majuzi juu ya. . .huko kwenye ule mkutano wa mwisho, juu ya kufanya kesi ya mahakamani. Naye Yesu akaleta, ama Mungu akaleta, kuhusu Neno Lake, kwa ajili ya kuvunja ahadi. Wengi wenu mmelisikia hilo. Na kwa hiyo nilikuwa nikiwazia juu ya labda kuileta hiyo, Jumapili alasiri, kesi hii ya mahakamani. Halafu wakili huyu hapa, huenda akaweza kunisahihisha juu ya baadhi ya utaratibu nitakaofuata.

4 Kwa hiyo, bali nikiketi hapa asubuhi ya leo, bila shaka ni ma—majaliwa. Nilikuwa nikiangalia kote, marafiki mbalimbali, kama mvulana mdogo hapa, maskini rafiki mmoja hapa, ndio kwanza aniite kule. Naye alikuwa amelemaa. Akasema, "Ndugu Branham, kama utaniambia tu kwamba ningeweza kutembea nitoke hapa, hilo tu ndilo ninalotaka ufanye." Mnaona?

Nami nikawazia tu, "Ni—ni la kupendeza jinsi gani!" Mnaona?

5 Lakini, mnaona, mambo haya ni tofauti kidogo na vile tunavyoninii. . .mnavyodhani yalivyo. Mnaona? Mnaona? Sasa, hapo ndipo ninapowazia wengi wa ndugu zetu wanaenda

kombo. Mnaona? Mnaona? Mungu atawaruhusu kufanya jambo fulani kwa imani ndogo. Ndipo wanajisikia kwamba kila kitu wanachorukia, wanakisema tu, na hiyo yatosha.

6 Lakini, mnaona, ninawezaje kusema BWANA ASEMA HIVI Yeye asiponiambia kwanza? Sina budi kuwa nalo kwanza. Kama sikuwa nalo, ningesema, "Hivi asema William Branham," bali hilo lisingefaa chochote. Lakini, mnaona, sasa, Yeye hana budi kuniambia kwanza.

7 Mtu fulani alikuja na gari la kuchukulia wagonjwa, pamoja na watoto wachanga. Nami nilikuwa na shughuli nyingi sana. Akasema, "Vema, mimi . . . Kama utaniambia tu; uje hapa na kusema mtoto wangu atakuwa mzima. Hilo tu ndilo ninalotaka kujua." Vema, hilo, jinsi lilivyo la kupendeza. Lakini ninawezaje kusema hilo mpaka nijue? Mnaona? Kama nikininii . . .

8 Watu wengine hufuata tu dhana, "Bwana aliniambia nifanye *hili*." Vema, hiyo—hiyo ni nafsi yako, mara nyingi. Mnaona? Inakubidi ulione kweli na ulijue.

9 Angewezaje—ningewezaje . . . Ndugu Fox hapa aseme kitu isipokuwa awe ni mkweli? Aseme, "Ndugu Branham alisema *hivi na vile*." Na kama sikusema hivyo, yeye—yeye—yeye ananisingizia kusema jambo ambalo sikusema. Bali kama kweli nililisema, basi sina budi kulitetea.

Kwa hiyo, Bwana anaposema lolote, hilo latosha.

10 Nilikutana na maskini Mbaptisti mmoja hapa muda mfupi uliopita. Na yeye si Mbaptisti. Nafikiri ni Mbaptisti Mpentekoste kama mimi. Na—naye ni maskini mkusini mwingine mwema. Nilimwangalia akila aiskrimu hii ya Georgia asubuhi ya leo hapa, ile, ya nafaka iliyokobolewa. Na kwa hiyo a—alikuwa ni mmoja wa wale wenye kung'ang'ania, mwajua. Naye alivuta sigara, na ni Mbaptisti mzuri sana, na hata hivyo . . . Kwa hiyo a—akaninii . . . naye alikuwa na mengi sana aliyokuwa akipitia. Naye akashikilia.

11 Sasa, hapa nje mkutanoni, ni wale, ninyi—ninyi watu. Watu, wanafanya hivyo, wenyewe. Mnaona? Na ni Kristo akiujia Mwili Wake. Mnaona?

12 Sasa, hebu nilipate hilo sasa hivi, nisimame pamoja nanyi kwa muda kidogo tu. Mnaona? Kristo akiujia Mwili Wake, hilo halimaanishi mimi tu. Mimi siye huo Mwili. Mimi ni mshirika tu wa Mwili huo. Mnaona? Ninyi ni sehemu ya Mwili huo, pia, "Kwa Roho mmoja." Wakorintho wa Kwanza 15 . . . Wakorintho wa Kwanza 12, "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Sisi ni washirika wa Mwili huo, kila mmoja wetu, kama wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mlutheri, wa umoja, wa uwili, wa utano, ama chochote ulicho nacho. Unaona? "Kwa Roho huyo mmoja sisi sote tumo kwenye Mwili mmoja." Kama Mungu akiwaruhusu wa umoja aingie ndani, pamoja na wazo lake la kipekee; church of God aingie, pamoja na wazo lake la

kipekee; Mmethodisti aingie, pamoja na wazo lake la kipekee; Mwassemblies aingie, pamoja na wazo lake la kipekee; hiyo ni juu Yake.

13 Ninao ndugu tisa, na kila mmoja wetu ni tofauti na mwingine, lakini sote tuna wazazi wale wale. Mnaona? Sisi, kila mmoja, ni wa Branham. Sasa, ndugu zangu . . . Mimi ni mwindaji. Ninapenda kuwinda na kuvua samaki. Hao wengine hawajali hayo. Wanapenda kucheza gofu na vitu kama hivyo, bali si mimi. Mnaona, huo ni upekee wangu. Lakini hata hivyo baba yao ndiye baba yangu. Mnaona? Bali sisi sote tunakubaliana, inapofikia habari za baba, kwamba ndiye baba yetu sote.

14 Na hivyo ndivyo tunavyofanya, pia. Sasa angalieni. Kanisa limekuwa, mnaona, linakua tu.

15 Kama tu vile nilivyokuwa nikitaka kuzungumza usiku wa leo, juu ya, "Kufunuliwa kwa yule Mungu mmoja wa kweli," bali nafikiri itachukua muda mrefu kupita kiasi. Ninaona watu, baada ya majira ya saa tatu, wanakosa utulivu. Niliwazia ningengojea tu mpaka wakati mmoja huko maskanini. Nina jambo lingine niani mwangu labda kwa ajili ya usiku wa leo, kuleta ujumbe wa wokovu. Huo ndio tunaojaribu. Huo ndio ninii wetu . . . kile tunachojaribu kufanya hapa.

16 Sasa, ninyi ndugu wahudumu, tuliukosa uponyaji wa Kiungu. Kama vile mzee Daktari Bosworth, ambaye ndio kwanza aende Nyumbani, Utukufuni, hapa chini, hivi majuzi. Alizoea kusema, "Uponyaji wa kiungu ni chambo unachoweka kwenye ndoana. Kamwe humwonyeshi samaki ndoana. Unamwonyesha chambo. Hu—humeza chambo akanaswa na ndoana." Kwa hiyo, hivyo ndivyo ilivyo. Sisi . . . Uponyaji wa kiungu huuvutia tu usikivu. Mnaona?

17 Na, halafu, wokovu ndio tunaotafuta. Tunazitafuta nguvu za Mwili wa Kristo. Mnaona?

18 Na kila moja ya madhehebu yenu mbalimbali, baadhi . . . Mimi siyapendelei sana madhehebu, ati kusema tu, "Mimi ni mfuasi wa *hili*."

19 Ni—niliwekwa wakfu, Mbaptisti. Halafu niliposikia habari za Wapentekoste, niliwazia, "Jamani! Ni nini hii?" Nikawazia, "Hao ndio nitakaojiunga nao." Nikaja huku. Wamegawanyika kama walivyo Wabaptisti, na kila namna ya mambo mbalimbali tu. Nao wote walikuwa . . . Nikawazia, "Vema, sasa, sitajiunga na lolote la hayo. Nitasimama moja kwa moja kati yao na kuwakumbatia wote, na kusema, 'Sisi ni ndugu.'" Na, mnaona, mfumo unaotuzuia kuwa hivyo, huo ndio ninaoupinga, mfumo, huo. Mnaona?

20 Na hiyo ndiyo sababu niko pamoja na kundi moja, na hilo ni la Wafanya Biashara wa Full Gospel. Mnaona? Tunataka kuitandaza hema yetu sana, itachukua kila kitu, wote hao,

mnaona, kila mtu. Sisi sote ni ndugu. Mnaona, kila mmoja wetu ni ndugu, katika Kristo. Sasa, mmoja wa wadhamini wa—wangu wakuu ni Waassemblies, na United, na Foursquare, na Church of God. Na ndugu hao wote, walitokea kuwa ni watu halisi.

21 Sasa, ni kitu gani? Kristo akiujia Mwili Wake. Kristo ni Neno. Sote tunajua upako ni Kristo, unaokuja juu ya Neno, unaolihuisha Neno. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Huo ndio upako. Kristo Ndiye upako huo, yule Roho anayekuja juu ya Neno, anayelihuisha Neno, kulifanya hai. Sasa, Neno limo moyoni mwako. Unaamini katika uponyaji wa Kiungu, chochote kile. Unaona? Naye Kristo, ule upako, akiujia Mwili Wake. Mnaona ule—ule uhusiano pale? Ni kama tu mume na mke kuwa mmoja. Sasa, kanisa halina budi kuingia kwenye huduma, mpaka kanisa na Kristo wawe kitu kimoja. Yeye anaweza kukutia mafuta kwa ajili ya kila baraka iliyo katika Biblia. Zote ni zako. Kila kitu kilichoahidiwa kwenye wakati huu ni chako. Tunapoacha chochote nje . . . Mnaona? Basi, kama upako ukiigusa hiyo, uta—utaitia mafuta. Iko tu hapa.

22 Kama vile, mi—mimi hutumia hili kama mfano. Lipo fundisho linaloitwa fundisho la piramidi. Bali kamwe usiingize hilo katika wazo lako, kwamba ni—kwamba ni—ninaamini mafundisho ya piramidi. Ninaiamini Biblia. Mnaona? Na, ingawa, ninaamini sehemu ya piramidi ilitumikia sehemu fulani kwake.

Ninaamini Mungu aliandika Biblia tatu.

23 Aliandika moja angani, ambayo ni zodiaki. Mtu yeyote anajua hilo. Ayubu alinena habari zake. Kitu gani? Hebu tazama zodiaki. Inaanza na bi—bikira. Inaishia kwenye Leo yule simba. Hivyo ndivyo Yeye alivyokuja, kwanza kwa bikira. Kuja Kwake kwa mwisho, kwingine, kutakuwa ni Leo yule simba, mnaona, akija kama Simba wa kabila la Yuda. Nao wote, basi, wale samaki waliokingama, tulio ndani yake sasa, wakati wa kaa, na kila kitu, yote yananena. Lakini, sahau hiyo. Mnaona? Hiyo siyo Biblia yenu.

24 Halafu, piramidi, jinsi hasa zilivyochorwa, jiwe la kuwekwa juu lilikataliwa. Bado, hiyo siyo Biblia yenu.

Halafu, Mungu akaiandika kwa Maneno.

25 Yesu anakuja mara tatu. Wakati mmoja, alikuja kumkomboa Mke Wake. Wakati huo mwingine, Yeye anakuja kumnyakua. Wakati huo mwingine, anakuja pamoja Naye. Kuja mara tatu. Mnaona?

26 Kila kitu, kama vile, “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” mnaona, vyote, kila kitu kiko katika utatu.

27 Hisabati ya Biblia ni kamilifu. Kama ukiziweka hizo hisabati sawa, unaweza kuiweka sawa hadithi yako. Mnaona? Bali ukienda kando ya hizo hisabati, utakuwa, katika picha

yako, na ng'ombe akila nyasi juu ya mti. Kwa hiyo, haita— haitaonekana sawa. Mnaona? Dumu kwenye hisabati, unaona, za Biblia, ndipo utaliweka sawa.

28 Sasa, nilikuwa nikizungumza juu ya jamaa huyu mdogo hapa, mwenye sura nzuri anayeketi hapa. Yeye, aliendelea kuja. Kila wakati, angeandikisha jina lake kwa ajili ya mahojiano ya faraghani. Vema, wakati angefanya hivyo, basi angengoja kwa muda mrefu, mpaka hatimaye wakati wake ukawadia. Huyu hapa anakuja.

29 Sasa, katika mahojiano ya faraghani si hivi, mnaona, sio kuketi mkutanoni kama tunavyofanya hapa. Utangojea mpaka Bwana atakaponena na kukuonyesha la kufanya.

30 Vema, kamwe haijaninii. . .Yeye kamwe hangeweza. . . Wakati wake ungekwisha. Vema, asingekata tamaa. Yeye aliandika tu jina lake apate mengine. Basi wakapita mamia kadhaa mpaka yakamfikia tena. Ndipo, siku moja, akiwa ameketi mahali pale. . .Angejaribu, angechukua mawazo yote ya saikolojia angaliweza, kuziacha hizo sigara, wala asingeweza kuziacha. Lakini siku moja ikaja, BWANA ASEMA HIVI. Hilo lilitosha. Huo ulikuwa ndio mwisho wake. Na kwa hiyo huyu hapa ameketi asubuhi ya leo. Naam. Kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya hilo.

31 Sasa, hebu nitoe maelezo madogo kwa dakika moja, kama ni sawa kuuchukua wakati hu—huu. Nafikiri. . .

32 Ninaiangalia saa pale. Saa nne, tunapaswa kuwa tumetoka, nilijua. Nilisikia kwa uvumi, dakika chache tu zilizopita. Nami ni kama tu treni ya mizigo; nachosha kwa maneno mengi.

33 Na—nakumbuka mara ya kwanza, nilipoanza kuhubiri. Nami nilikuwa ni mhubiri mdogo, Mbaptisti. Ningeibeba Biblia hiyo chini ya kwapa langu, nami nilidhani nilikuwa mhubiri tu halisi. Mtu fulani akisema, "Je! wewe ni mhubiri?"

Ningesema, "Hakika. Naam, bwana, kweli kabisa."

34 Basi inanikumbusha wakati nilipokuwa mvulana, huko mashambani. Ba—babangu alikuwa mpanda farasi. Naye angewafunza farasi na kufuatilia mashindano ya wachunga ng'ombe, akawafundishe farasi, na kadhalika. Kwa kweli alikuwa mpanda farasi mzuri. Vema, nikawazia, kwa kuwa mimi ni mwanawe, kweli nilikuwa mpanda farasi, pia. Kwa hiyo ningeninii. . .baba angekuwa huko mbali nyuma ya shamba, pamoja na farasi wake, mwajua. Nami ningemtoa maskini yule farasi mkongwe wa kulima, mwajua, mkongwe na amepinda, ameshupaa na ni mchovu.

35 Nasi tulikuwa na kihori cha kale kilichochongwa kutokana na gogo la mti. Ni wangapi wamepata kuona kimoja cha hivyo? Vema, kwani mmetoka sehemu ipi ya Kentucky, hata hivyo? Na

kwa hiyo . . . Nasi tulikuwa tukiteremka pale na kudungwa na nyuki wa asali, mwajua, wakija kunywa maji yao na kadhalika.

36 Kwa hiyo, ningetazama na kumwona baba akifanya doria yake, kupitia shamba la mahindi, huko nyuma kabisa. Ningenyemelea ndani na kuchukua tandiko lake, na kovu la magugu yenye miiba, mwajua, na kuyachomeka chini ya tandiko hilo, nikavuta mkanda wake, na kumpanda. Basi maskini farasi huyo mkongwe! Ndugu zangu wadogo wameketi karibu pale, wangeshangilia, "Mwendeshe, Billy! Mwendeshe!" Mwajua, naye maskini farasi huyo, amechoka sana, asingeweza hata kuinyanyua miguu yake kutoka ardhini, mwajua, "pump, pump." Nikawazia, "Jamani, mimi ni mpanda farasi!" Nilikuwa nimesoma hadithi nyingi kupita kiasi za Kimagharibi. Hayo tu. Kwa hiyo ni—nikawazia, labda, mwajua, vema . . . Mwajua, ninaninii . . .

37 Siku moja niliamua kwamba walinihitaji huko Magharibi, kuwafunza farasi wao, mwajua. Basi, mimi, mwenye umri wa miaka kumi na minane hivi. Iliwabidi wanichukue. Huduma za—zangu zilihitajika, kwa hiyo niliponyoka moja kwa moja nikaelekea Magharibi.

38 Nami nikajaribu kujinunulia surupwenye. Nilikuwa jamaa mdogo, mwajua. Nami nilidhani ilikuwa na ninii sana . . . ilikuwa imeandikwa A-r-i-z-o-n-a na kuchorwa kichwa cha maksai. Sasa, "Loo, jamani! Hiyo inapendeza." Nilipoivaa, nilionekana kama mmoja wa hawa kuku wa mchezo, mwajua, na hayo manyoya yote. Nisingeweza kutembea na vitu hivyo, kwa hiyo nikajinunulia tu suruali ya—ya Levis.

39 Nikawazia, "Vema, nitakalia matandiko ya fedha. Nitatoka niende nikajinunulie ninii . . . Nitaketi kule na kungojea mpaka watakapowatoa farasi dume. Kuna baadhi ya hao jamaa wanaorushwa; nitawaonyesha jinsi ya kuwapanda. Babangu ni mpandaji."

40 Kwa hiyo, nikapanda kwenye uzio. Walikuwa wakiwafunza farasi wengine. Ndipo nikaangalia pale kizimbani, na kuwaona hao maharamia mle ndani, ambao, jamani, hata usingemrushia nyasi kavu. Walikuwa ni wakorofi sana, wasingeila. Kwa hiyo, nikawaza, "Aisee, sijui. Huyo haonekani kama maskini yule farasi mkongwe wa kulima niliyempanda." Kwa hiyo nikamtazama kwa kitambo kidogo.

41 Baada ya kitambo kidogo, walikuwa na mmoja pale waliyemwita, "haramia wa Kansas." Kwa hiyo wakamleta, farasi mkubwa mno mzito, yapata mikono kumi na saba mle. Alikuwa farasi kwelikweli. Kwa hiyo wakaweka ninii . . .

42 Kulikuwako na mtu mzuri pale, akiwa amevalia nguo yake rasmi iliyo nzuri sana, na kadhalika; wasichana wote wakimpungia mikono. Alikuwa ni nyota kwelikweli. Nilimwangalia wakati akitoka kwenye gari lake. Wakasema,

"Mtu huyu anaweza kumpanda farasi huyu." Kwa hiyo, wakamweka kwenye mwavuli. Naye akapanda pale, na kujiandaa, akaketi kwenye tandiko lake.

43 Wakafungua lango. Jamani! Loo, jamani! Yapata misokoto miwili na madoadoa, naye alionekana kana kwamba angelirusha tandiko hilo juu ya mwezi. Sijapata kuona kitu kama hicho! Vema, pikapu ikamchukua farasi na gari la kuchukulia wagonjwa likamchukua mpandaji.

44 Huyu hapa mwitaji anakuja huku, mwajua. Akasema, "Nitampa mtu yeyote hapa, dola mia tano, anayeweza kusalia juu yake sekunde sitini."

45 Akashuka moja kwa moja kwenye foleni. Sijui ilivyokuwa kamwe, akanichagua moja kwa moja. Nimeketi pale, nimeketi pale pamoja na huyu kaoboi aliyeumbuka, mwajua. Miguu yangu haikuwa na matege, wala chochote kile. Lakini ni—nilifikiri nilikuwa mpandaji halisi, ningeweza kuketi pale pamoja nao. Nilikuwa nikishiriki pamoja nao, mwajua, huku kofia yangu imekaa nyuma ya kichwa changu. Nilikuwa na yapata umri wa miaka kumi na saba, nadhani, nikiangalia kote namna *hiyo*. Akaja, kasema, "Je! wewe ni mpandaji?"

Nami nikasema, "La, bwana."

46 Nilikuwa mhubiri mdogo wa Kibaptisti, nilikuwa nikiwazia Mungu aliniita kuwa mtetezi wa Neno. Mnaona? Alikuwa aitetee i—imani. Siku moja nilikuwa huko St. Louis, Missouri, nami nikaingia kwenye mkutano wa hema, ndipo nikakutana na Robert Daugherty. Yeye ni mhubiri Mpentekoste. Niliketi jukwaani pamoja naye. Jamani, mtu huyo alihubiri mpaka anakuwa bluu usoni, na kugonganisha magoti yake pamoja, na kuzuia pumzi yake. Ungeweza kumsikia umbali wa mijengo miwili ya mji. Kisha anarudi akihubiri. Ndipo mtu fulani kasema, "Je! wewe ni mhubiri?"

47 Nikasema, "La. Bwana." Mimi huchangamana na Wapentekoste; sisemi mengi kuhusu kuwa mhubiri. Nilikuwa kwa hilo kama ilivyokuwa kwa yule farasi. Mnaona? Ninasema tu, "La. Bwana aliniita nipate kuwaombea watoto Wake wagonjwa." Kwa hiyo ninaninii . . . Mnaona?

Kwa hiyo tuna—tuna furaha kuwa hapa asubuhi ya leo, kwenye hili.

48 Wakati tukiwa kwenye wazo la kupanda farasi; ninapenda mazingira ya porini. Huko ndiko nilipokutana na Mungu. Nami nilikuwa nikichunga mifugo kiasi, Colorado, kupanda huko juu. Sasa, kwa kawaida mimi hupanda farasi nikiwakusanya ng'ombe, na kadhalika. Tulikuwa na ninii . . . kule juu kwenye Mto Msumbufu. Sasa, mara nyingi nimesimama pale kando ya lango, wakati tukiwakusanya ng'ombe, mkusanyo wa msimu wa kuchipuka majani kuwapandisha ng'ombe. Shirika la Hereford huwalisha kwenye bonde hilo. Unachangia tani mbili za nyasi

kavu; unapata haki, ama ranchi yako, ya kumpeleka ng'ombe msituni. Na baadhi yao wana mamia ya ng'ombe, maana wana mahali wanapoweza kufanya umwagiliaji maji huko chini. Wana malisho hayo mwitu. Halafu kuhusu . . .

49 Kila msimu wa kuchipusha majani, wanapowapeleka hao ng'ombe kule juu mwituni, a—askari mpanda farasi husimama pale na kuwahesabu ng'ombe hao, na kuchunguza alama zao. Hao, kila mmoja, ametiwa alama. Lile kundi dogo nililolifanyia kazi halikuwa na wengi sana, yapata ng'ombe mia moja na hamsini, mia mbili, maskini mifugo wa alama pembe tatu. Na Masizi, Mkuo, Mkuo wa Almasi, walikuwa na yapata ng'ombe elfu moja mia tano.

50 Bali kuna kitu kimoja nilichoona sikuzote, wakati nimesimama pale. Baada ya kuwapeleka ng'ombe kule juu, na askari mpanda farasi amesimama kwenye uzio wa kuhamishwa. Huo ni wa kuwazuia ng'ombe kuingia kwenye mali ya mwenyewe tena. Nilikuwa nikiketi pale na kuweka mguu wangu kwenye ncha ya tandiko na kumwangalia askari huyo. Naye angewaangalia hao ng'ombe wakati wakiingia, anasimama pale. Kila ng'ombe aliyeingia, ilikubidi kumkagua. Unaona, hakushughulika sana na alama waliyokuwa nayo. Bali kuna kitu kimoja ambacho alikichunguza kwa makini, hicho kilikuwa ni kishikizo cha damu. Mnaona? Kwa sababu, huwezi kuweka kitu chochote mle ndani kwa ajili ya ukoo, kuhifadhi u—ukoo uwe sawa. Mnaona? Hakuna mwingine ila Hereford halisi angaliweza kuingia kwenye mbuga hiyo; mbuga hiyo, hakuna mwingine ila Hereford. Ilibidi awe na kishikizo cha damu, kuonyesha ya kwamba alikuwa amekaguliwa. Naye alikuwa na kishikizo cha damu, kuonyesha ya kwamba alikuwa ni Hereford.

51 Nafikiri hivyo ndivyo ule mkusanyiko mkuu utakavyokuwa. Yeye hatatuuliza kama sisi ni Waassemblies, ama kama sisi ni wa Foursquare. Yeye ataangalia kile kishikizo cha Damu, haijalishi kuhusu kibandiko chetu. Tutachunguza kishikizo cha Damu. "Ninaiona Damu."

52 Mimi, nina furaha sana kuhusishwa na watu kama hao asubuhi ya leo. Bwana awabariki sana sasa. Nikiketi na kuzungumza nanyi; wakati wangu ungekwisha.

53 Ninataka kusoma Neno la Bwana, kwa kuwa hakuna ibada iliyo kamili pasipo kusomwa kwa Neno. Sasa hebu tuyafungue Maandiko hapa pamoja na mawazo machache niliyokuwa nimepanga.

54 Huko nyuma ilikuwa kawaida, ilikuwa kwamba ningeweza kukumbuka mambo ambayo nitasema, pasipo hata kuandika muhtasari. Lakini tangu nilipopita umri wa miaka ishirini na mitano, mara ya pili, siwezi kuyakumbuka kama nilivyokuwa nikifanya. Kwa hiyo kwa namna fulani inanibidi kuandika

muhtasari, kuandika fungu langu, yale nitakayosema, na kuyakumbuka. Kisha pia ninakumbuka, mengine zaidi.

55 Nilikuwa mtoto wakati huo. Nilitatarika tu, kama vile kupiga bunduki ya marisau. Mnaona? Lakini sasa inakubidi kupanga mawazo. Watu walikuja kunisikia kwa kuwa nilikuwa tu ni mvulana mhubiri. Hii ni miaka thelathini na mitatu nyuma ya mimbara kwangu. Lakini sasa ninakutana na watu mashuhuri, kama nilioketi mbele zao asubuhi ya leo. Inakubidi kulenga shabaha. Inabidi iwe ni Neno.

56 Namkumbuka mzee mhubiri wa Kibaptisti aliyeniweka wakfu. Ninakumbuka mara yangu ya kwanza niliposimama kuhubiri. Nililia tu na kugongagonga dawati, na kila kitu namna hiyo. Na baadhi ya wanawake wakongwe wakaja pale na kunipapasapapasa mgongoni, kasema, "Loo, kipenzi," huku wanalia. "Utakuwa mtumishi mkuu wa Kristo."

57 Mzee Dk. Davis ameketi pale, alikuwa amenikazia macho. Nikasema, "Nilifanyaje, Dk. Davis?"

58 Kasema, "Mabaya sana niliyopata kusikia maishani mwangu." Alinikemea. Kwa hiyo alikuwa ni wakili. Kwa hiyo a—akaniambia, baadaye, kasema, "Njoo kwenye chumba changu cha kusomea, Billy." Akasema, "Billy, mhemuko wako wote, na yote uliyopitia," kasema, "ulikuwa tu ukijaribu kutenda kama mhubiri." Akasema, "Ni—nilifanya vile vile nilipofanyika wakili." Kasema, "Mimi . . . Kesi yangu ya kwanza ilikuwa ni kesi ya talaka, na," kasema, "kweli haikuwa na misingi kabisa. Lakini," kasema, "nilimwambia maskini mwanamke huyu . . . Nililia, na kukimbia na macho yangu." Kisha akasema, "Mimi . . . Maskini mwanamke huyu, mume wake alifanya *hivi-na-hivi* na kadhalika."

59 Kisha kasema, "Nilipata kitu kile kile nitakachokupa, nami niliwazia ni kitu kizuri." Kasema, "Jambo la kwanza wajua, ninii . . . Kwa hiyo yule wakili mwingine aligonga dawati na kusema, 'Hakimu, mheshimiwa, bwana, mahakama yako itavumilia kiasi gani zaidi upuuzi huu?'" Mnaona? Kasema, "'Hajasema jambo moja kumtetea mtu huyu, bado, si hata kipengele kimoja cha sheria. Yeye analia tu na kurukaruka.'" Akasema, "Unajua nini? Hilo lilizimisha kabisa majivuno yangu nikajirudia." Kasema, "Sasa, Billy, ulikuwa ukiingiwa na mihemuko yote, ukilia na kurukaruka, bali kamwe hukuleta kipengele kimoja cha Maandiko ambacho kweli kinaleta mambo ya kimsingi, kwa ajili yake." Hiyo ni kweli.

60 Sasa tunatupa risasi. Haina budi kulengwa. Haina budi kupiga mahali penyewe. Bwana tusaidie sasa tunapolisoma! Kutoka Yoshua, mlango wa 10. Nami nitaanzia kwenye kifungu cha 12, na kusoma Yoshua 10:12 kufikia kifungu cha 14 ama 15.

> *Ndipo Yoshua akanena na* BWANA *katika siku hiyo ambayo* BWANA *aliwatoa Waamori mbele ya wana wa*

Israeli; akasema mbele ya macho ya Israeli, Wewe, Jua, simama . . . kimya juu ya Gibeoni; nawe Mwezi, simama katika bonde la Aiyaloni.

Ndipo jua likasimama, na mwezi ukatulia; hata hilo taifa lilipokuwa limekwisha kujipatiliza juu ya adui *zao. Hayo je! Hayakuandikwa ndani ya kitabu cha Yashari? Basi jua likasimama kimya katikati ya mbingu, wala* halikufanya haraka *kuchwa, kama muda wa siku nzima.*

Haikuwako siku nyingine mfano wa siku hiyo . . . wala baada yake . . . hata ikawa yeye Bwana *kusikia sauti ya kibinadamu, kwa kuwa* Bwana *alipiga vita kwa ajili ya Israeli.*

61 Sasa, kama mtanisamehe kwa dakika moja, ninataka kuchukua fungu hapa asubuhi ya leo, juu ya somo la neno moja.

62 Sasa, mnasema, "Ndugu Branham, hilo si—hilo si kubwa sana kwa kusanyiko hapa, watu mia moja na hamsini ama kitu kama hicho. Hilo—hilo halitoshi." Loo, naam, limetosha. Li—limetosha. Ni Neno la Mungu. Mnaona? Haidhuru, ni—ni—ni . . . Sio ubora; ni wingi.

63 Kama vile hapa, si muda mrefu uliopita, katika Louisville, Kentucky, nilikuwa nikiwazia juu ya mvulana mdogo aliyepanda darini, alikuwa akipekuapekua, siku moja. Ndipo akapata katika upenu wa kale, katika kasha dogo akapata stampu ya posta. Basi akawaza, "Mwajua, huenda hii ikawa na thamani fulani." Kwa hiyo akatimua mbio akampata mkusanyaji. Na, hakika, alikuwa anawaza juu ya aiskrimu. Kasema, "Utanipa nini kwa ajili ya stampu hii?"

64 Akasema, "Vema, ni—nitakupa dola moja kwake." Loo, jamani, hiyo ilikuwa ni kama koni kumi pale, mwajua, kwa hiyo a—alikuwa amefikiria amepata bei nzuri.

65 Mtu huyo akaiuza, baadaye kidogo, kwa dola mia tano. Nami nasahau sasa, imefikia maelfu, thamani ya stampu hiyo. Mnaona, kuhusu karatasi, haikuwa na thamani yoyote. Bali ni kile kilichoandikwa juu yake, ndicho kinacholeta tofauti.

66 Hii ni karatasi tu nyembamba sana ya kawaida. Ila ni kile kilicho juu yake. Ni Mungu katika herufi. Mnaona? Naam. Wakati mwingine ni ninii . . . Haidhuru ni dogo jinsi gani . . .

67 Hapo ndipo sisi watu hufanya kosa letu. Daima tunatamani kufanya jambo kubwa. Labda hatukuchaguliwa kufanya jambo kubwa. Labda ni mambo madogo tunayoacha bila kufanya ndiyo yanayotudhuru.

68 Kama vile huko Kanada, nilikuwa nimesimama kule na rafiki yangu mpendwa, Dk. Ern Baxter, ambaye alikuwa mtu wangu wa jukwaani; mtu mzuri sana, msemaji hodari sana. Na wakati . . . Mfalme George, ambaye nilikuwa na majaliwa ya

kumwombea, mwajua, hapo alipoponywa ugonjwa wa kushupaa mifupa. Wakati yeye na mkewe walipopita mtaani siku hiyo huko Vancouver, walipokuwa wakishuka kwenda mtaani pale. Alikuwa amevaa nguo yake nzuri ya bluu. Naye mfalme mwenyewe ameketi pale, akijaribu kukaa sawa, anaumwa na ni mgonjwa, vidonda vyake vikimsumbua. Bali hata hivyo alijua yeye alikuwa ni mfalme, kwa hiyo akawasalimia watu. Na wakati alipopitia hapo, mimi na Ern tulisikiliza. Yeye. . . Ern alikigeuza tu kichwa chake akaangua kilio. Asingeweza kujizuia. Akasema, "Ndugu Branham, mfalme wangu anapita."

69 Nikawazia, "Kama itamfanya Mkanada kujisikia namna hiyo, itafanyaje sisi tutakapomwona Mfalme wetu akipita?"

70 Waliwaachilia, watoto wote, kanisa, ama shule ziliachiliwa, wakamwone mfalme. Wakawapa bendera ndogo za Kiingereza, wakazipeperushe. Waliporudi shuleni, baada ya utaratibu wao wa kawaida, walikuta kwamba jamaa mmoja mdogo hakurudi. Basi mwalimu akashtuka, kwa hiyo akatoka kwenda kumtafuta jamaa huyo mdogo. Naye alikuwa amesimama, msichana huyo mdogo alikuwa amesimama nyuma ya nguzo, akilia kwa uchungu mwingi. Mwalimu akamtwaa akasema, "Kuna nini, kipenzi?" Kasema, "Hivi hukumwona mfalme?"

Akasema, "Naam, nilimwona mfalme."

Ndipo kasema, "Ulipeperusha bendera yako ndogo?"

Kasema, "Ndiyo, niliipeperusha bendera yangu ndogo."

Kasema, "Unalia nini?"

71 Akasema, "Unajua," akasema, "mimi ni mdogo sana." Akasema, "Na—nalimwona mfalme, na nikaipeperusha bendera yangu, lakini mfalme hakuniona." Mnaona? Basi maskini moyo wake ulihuzunika.

72 Hiyo ni tofauti na Mfalme wetu. Usingeweza kuwa mdogo sana; huwezi kufanya lolote. Ye—Yeye huona kila hatua ndogo unayochukua. Anajua yote kukuhusu.

73 Sasa, somo langu asubuhi ya leo, nitakalolizungumzia kwa dakika chache, Bwana akipenda, ni: *Kitendawili*.

74 Kitendawili ni nini? Kulingana na Webster hapa, kinamaanisha, "kitu ambacho hakiaminiki bali ni cha kweli." Nafikiri tumeshuhudia hilo, siku chache zilizopita, kiwango hiki kidogo. Lakini, *kitendawili*, kitu "kisichoaminika, bali hata hivyo ni kweli." Hilo linafanya kitendawili.

75 Katika Waebrania, mlango wa 11 na kifungu cha 3, tunaona ya kwamba ulimwengu ulifanywa na kuundwa kwa Neno la Mungu.

76 Majuma machache yaliyopita, nilikuwa katika Jiji la New York kwenye Jumba la Mikutano la Morris. Nikaisikiliza kanda hii ya—ya Einstein ikizungumza juu ya kundi lile la nyota,

kwamba ni ngapi. . .Kama tungaliondoka hapa na kwenda, nafikiri, miaka milioni mia moja hamsini ya mbio za nuru, tukisafiri kwa mwendo wa nuru, itatuchukua miaka milioni mia moja na hamsini ya nuru kufika kule, halafu miaka milioni mia moja na hamsini ya nuru kurudi. Sasa, mnajua jinsi nuru husafiri upesi. Mnaona? Na, wazieni tu, miaka milioni mia moja na hamsini ya nuru. Vema, kama ungalichora safu za tisa kuzunguka, kuzunguka, kuzunguka dunia, usingeweza kuziweka katika miaka. Tisa, tisa, tisa tu, zimekaribiana, kuuzunguka ulimwengu, usingeweza kuziweka katika miaka. Kwa maana, wazia tu, nuru husafiri. . .Ni kitu gani? Maili mia nane, nane. . .mia moja themanini na sita. . .mia—maili mia moja themanini na sita elfu kwa sekunde. Na mwa—mwaka wa nuru? Katika miaka milioni mia tatu ya nuru, hebu jaribuni kupiga hesabu hiyo. Nawe unajua huo ni muda gani basi, tungekuwa tumeondoka duniani? Miaka hamsini. Hiyo ni kweli. Mnaona?

77 Walivunja wakaingia, wapate kuuona, Umilele. Wanasema ya kwamba John Glenn, yule mwanaanga aliyezunguka, haikuondoa sekunde moja kutoka maishani mwake, hata kwenye mwendo aliokuwa akisafiri, yapata maili elfu moja mia saba. Mnaona? Kwa hiyo basi, mnaona, tulivunja tukaingia katika Umilele. Sisi ni watu wa duniani wanaojua tu inchi na kadhalika. Unapovunja ukaingia huko kusikojulikana, u—usingeweza kung'amua hilo. Akili zetu si pana vya kutosha. Sisi, tusingeng'amua. Tusingeng'amua maana ya kuingia kwenye huo, bali tunajua kwamba ni kweli.

78 Naye Einstein alisema, "Kuna jambo moja tu la maana la kusema juu ya ulimwengu. Kwa imani tunafahamu ya kwamba Mungu aliuumba ulimwengu." Mnaona?

79 Nao ulimwengu, ukisimama pale angani, ilibidi utoke mahali fulani. Sayansi inasema ni kipande cha jua. Basi jua lilitoka wapi? Mnaona, unaendelea kuivunjilia mbali, mpaka hatimaye unafikia mahali ambapo huna budi kujua, ilibidi iwe na mwanzo. Mnaona? "Mungu aliumba mbingu na nchi," tunafundishwa katika Biblia. Nayo inasimamaje angani? Haisogei kamwe. Huwezi. . .

80 Huwezi kuchukua chombo. . .Nimevaa, kutoka kwa Ufini wangu, mikutano yangu katika nchi za ng'ambo, na Uswisi, moja ya saa zao nzuri kuliko zote nilizopewa, wakati nilipokuwa kule. Kweli ni ninii. . .Nafikiri, katika hela za Marekani, inagharimu dola mia moja na hamsini, mia mbili, labda zaidi. Na hata hivyo saa hiyo itaongezea ama kupoteza, katika siku chache tu. Niliipeleka kwa muuza vito. Akasema, "Vema, hatuna kitu kinachouweka kikamilifu." Mnaona?

81 Bali ulimwengu huuweka, kikamilifu, kwenye wakati wake. Wanaweza kujua kupatwa kwa jua na kwa mwezi, miaka mingi,

mingi awali, kufikia kwenye dakika moja. Jinsi unavyopinduka, hata hivyo hakuna kitu kinachoushikilia.

82 Ni ipi iliyo juu na ni ipi iliyo chini? Hatujui. Je! Ncha ya Kaskazini iko juu, ama Ncha ya Kusini ndiyo iliyo juu? Tuko angani. Hicho ni kitendawili, sivyo? Hakiwezi kuelezeka. Chochote ambacho—ambacho hakiwezi kuelezeka namna hiyo, kwa urahisi ni kitendawili. Kwa hiyo tunaona ya kwamba ilikuwa ni kitendawili kwa ulimwengu kuwa—kuwa angani. Vema.

83 Na wakati na majira, unapitaje majira yake kwa wakati ule ule? Jinsi ambavyo, msimu wa kiangazi na wa baridi kali . . . Jinsi unavyoinama, huinama kinyumenyume. Kama ulikuwa umesimama wima . . .

84 Sasa, tulithibitisha hilo, wakati mmoja, ulikuwa umesimama wima, kama vile Mungu alivyosema ulisimama. Huko, yale maeneo ya barafu ya Kiingereza, wanaweza kulipua futi mia tano kupitia kwenye hiyo barafu, kuna mitende, kangaga, zinazoonyesha kwamba ilikuwa nchi ya joto wakati mmoja. Na sasa, mnaona, imeinama nyuma. Kutokana na yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika, iliinama nyuma. Nami ninaamini, kile kitu hasa kilichoirusha ikatoka kwenye duara yake wakati huo, kiko tayari kuirudisha kwenye duara yake sasa.

85 Mwanadamu hujiangamiza mwenyewe kwa maarifa yake. Mnaona? Kamwe haninii . . . Mungu haangamizi chochote. Mwanadamu . . . Nawe . . . Hatuwezi. Haidhuru tu—tunaweza kufilisi nini, tusingeweza kuangamiza kabisa. Hakuna kitu. Na hata moto ndio tulio nao karibu sana wa kuangamiza, bali huwezi kuangamiza. Wakati mioto inawaka, hizo ni gesi zikivunjika-vunjika. Hurudi moja kwa moja kwenye asili yake tena. Huwezi kuangamiza chochote. Watu wengine hushikwa na hatia sana hata wanataka ku—kuuchukua mwili wao ukachomwe moto, na kuupulizia kwenye pepo saba za baharini. Bali hilo halileti tofauti yoyote. Ninii wako . . . Haujaangamizwa. Huwezi kuangamiza. Mungu aliuumba. Huwezi kuurarulia mbali . . . Unaweza—unaweza kupotosha na kufanya vurugu, ama kufanya mambo mengine, bali huwezi kuangamiza. Mungu Ndiye tu anayeweza kuangamiza. Yeye Ndiye muumba. Ndiye pekee aliye na haki ya kufanya hivyo.

86 Jinsi unavyosimama angani! Tungalisema mengi sana juu ya hilo, tuchukue saa kadhaa juu yake. Lakini tunaona hapa ya kwamba Yoshua, akilisimamisha jua, sasa, hicho ni kitendawili.

87 Ninakumbuka wakati ambapo mzee baba yangu, hakuwa na elimu, nami . . . Ilikuwa ni vigumu kwake kuandika jina lake. Lakini alikuwa akiniambia, akasema, “Unajua, nisingeweza kuamini kwamba—kwamba, ila kwamba jua huzunguka, kwa ulimwengu.”

Nami nikasema, “Vema, sijui, baba.”

88 Siku moja kwenye shule ya sekondari, ninajua nilikuwa nikizungumza na mwalimu wa shule ya sekondari pale, juu—juu ya Biblia, na—na nikamwuliza swali hili kuhusu Yoshua. Akasema, “Kuzunguka kwa dunia kulifanya nguvu za uvutano, nazo nguvu za uvutano zikaushikilia u—ulimwengu juu.”

89 Nami nikasema, “Basi, kwa nini basi, (mnaifundisha Biblia), je! Yoshua aliliamuru ju—jua kusimama kimya?”

90 Akasema, “Mungu alijifanya kama haoni ujinga wake, unaona, na kuisimamisha dunia.”

91 Nikasema, “Ndiyo kwanza umalizie kuniambia . . . ” Sasa, yeye hakuamini miujiza ya Mungu. Mnaona? Ndipo akasema . . . “Ndiyo kwanza umalizie kuniambia, ‘Kama dunia ingalisimama kamwe, ingesimamisha nguvu zake za uvutano, basi ingevurumishwa kama kimondo kupitia hewani.’” Nikasema, “Biblia ilisema ya kwamba dunia ilisimama kimya hapa kwa muda wa saa ishirini na nne.” Mnaona? Mnaona?

92 Ni kitendawili. Lakini, Mungu alifanya hivyo, haidhuru, (nini?) kwa mwanadamu; sio mungu fulani, sio Malaika mkuu akishuka kutoka Mbinguni; mwanadamu, akiwa na imani katika huduma aliyopewa, kuiteka nchi hiyo. Neno la Mungu lilikuwa nyuma yake, “Ninawapeni nchi hii. Na kila mahali nyayo za mguu wako zitakapokanyaga, hapo nawapa. Ni penu.” Nyayo za miguu zilimaanisha umilikaji. Nalo jua ndilo . . .

93 Ma—mafanikio aliyokuwa akijaribu kupata! Mnaona? Adui wake alikuwa ameshindwa, naye alijua, kama jua likitua kamwe, hao wafalme wangeungana na kumshambulia kwa nguvu maradufu. Kwa hiyo, jua lilikuwa likiteremka, naye Yoshua, mwanadamu, akaagiza hili litendeke. Kasema, “Jua, simama kimya.”

94 Chochote kile Mungu alichofanya, sijui mimi. Ila jua lilisimama kimya, mwezi juu ya Aiyaloni, kwa maana mtu, mwanadamu, mwanadamu alikuwa kazini. Kazini, aliliamuru jua kusimama kimya. Na kama sisi ni Wakristo, hatuna budi kuamini kwamba Hili ni Neno lisilokosea la Mungu, kila mahali. Yeye aliisimamisha dunia, akalisimamisha jua. Chochote alichofanya, lilisimama kimya kwa muda wa saa ishirini na nne. Ninaamini hilo.

95 Yesu alisema, katika Marko Mtakatifu 11:22, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.”

96 Lakini hilo linahitaji nia na kusudi. Bila shaka, huna budi kuwa na sababu kwa ajili yake. Huwezi kuwa na imani isipokuwa uwe una sababu fulani. Kama nilivyojaribu kusema jana usiku, imani ya watu wengine imo kwenye kitabu chao cha kiada, imani ya watu wengine imo kwenye kitu kingine, bali inategemea imani yako ilipo. Ninataka kuliamini Neno la Mungu, kile anachosema ni kweli. Kisha sina budi kuona kama

ni mapenzi Yake ama siyo. Halafu, endapo ni mapenzi Yake, sina budi kuchunguza kusudi langu kwalo, halafu nia yangu katika kulifanya.

97 Kama nikilifanya kwa sababu ninasema, "Vema, ninaenda juu ya mlima hapa. Kuna mlima mbele zangu. Kuna watu milioni moja upande ule, wanaoangamia. Nina milioni mia moja hapa ninaowahubiria." Vema, kama siwezi kuupanda, kuuzunguka, wala kupitia chini ya mlima huu, wala chochote kile, na hata hivyo kitu fulani moyoni mwangu kinaendelea kuniambia, "Kwea mlima huu. Waendee. Waendee," wala siwezi kuupanda. Sasa, Yesu alisema, "Watauhamisha mlima huu." Mnaona? Ikiwa . . .

98 Sasa, jambo ni kwamba, kwanza, vipi kama nikisema . . . Sasa, kwanza, kamwe—kamwe sikuumba kile mle ndani. Kitu fulani kilikiumba. Ni kwa kusudi jema. Kwa sababu, kwa nini niwaendee milioni moja, wakati milioni mia moja hapa, wanaangamia upande huu? Lakini ni kitu fulani moyoni mwangu, kikisema, "Nenda upande *ule*."

99 Sasa, jambo la kwanza, itanibidi kusema, "Vema, kama nikienda kule, upande *huu* unaweza tu kunilipa kiasi *fulani* kwa mwezi. Na kule, hao . . . ." Mnaona, kusudi langu si zuri. Nia yangu si nzuri. La.

100 Vema, vipi kama nikisema, "La, sijali juu ya pesa. Lakini nitakapofika huko, siku moja, nya—nyakati zijazo, watajenga kumbukumbu kubwa mno, isemayo, 'Ndugu Branham, yule mmishenari mashuhuri.'"? Ndipo basi, bado, kusudi langu si zuri.

101 Lakini wakati sijali kamwe kama watajua ni nani aliyeenda kule, "Yeye yumo tu moyoni mwangu," basi nitaunenea mlima huo. Itatendeka. Mnaona? Haina budi kutendeka.

102 Lakini, unaona, nia yako na kusudi lako linategemea wewe ni nani na una shughuli gani. Kwamba ninii yako . . . Kitu gani? Hapo ndipo kanisa hulikosa, kufikia wakati huu. Wanasisimka katika mhemuko, na, punde si punde mwajua, katika shauku, hutulii ukalichunguza Hapa tena. Chunguza Hapo, kwa hakika, ndipo ni BWANA ASEMA HIVI. Angalia kama ni kweli.

103 Yoshua alikuwa na agizo la kwenda kule na kuiteka nchi hiyo, ndipo Mungu akasababisha kitendawili kikuu. Hata sayansi inaweza kuthibitisha, leo, kovu lingali angani, ambapo hilo lilitukia kikamilifu. Nilisikia huko Chicago, si muda mrefu uliopita, mwanasayansi akizungumza, ambaye alikuwa akilionyesha kwenye chati ndogo, ambapo lilitukia.

104 Sasa tunaona, tena, Musa alikuwa kazini, pia. Na kulikuwako na Bahari ya Shamu.

105 Mliona yale makala ya kijinga ambayo watu wengine wanajaribu kuyafanya sasa, kwamba Musa alipitia kwenye

lu—lundo la manyasi, bahari ya manyasi? Hilo si lilikuwa ni baya sana? Kujaribu tu. . . Ibilisi akiwavuvia watu hao kuiondoa Kweli ya Neno. Hayo maji yangewezaje . . . Halafu basi kwani manyasi yalimzamisha Farao majini wakati alipokuja? Ni wazimu. Mnaona?

106 Ndipo tunaona ya kwamba Musa alikuwa na agizo la kuwatoa hao watu Misri, kuwapeleka kwenye mlima ule. Nao hao hapo, kazini. Ndipo Musa akaanza kumlilia Mungu, wakati alipoiona ile Nguzo ya Moto ikining'inia hapa juu. Ndipo yakaja magari ya Farao. Naye akalia. Ile Ngu—Nguzo ya Moto ikashuka, ilikuwa ni nuru *kwao*, na giza kwa *hao*. Ndipo Mungu akasema, "Kwa nini unanililia? Nilikuagiza kufanya hayo. Nena na usonge mbele." Loo, jamani!

107 Shida ni kwamba, leo, makanisa yanazungumza, inaonekana, yanasema, "Moody alisema nini? Sankey alisema nini?"

108 Nena ukaseme yale Mungu aliyosema. Shime tusonge mbele, si kuangalia nyuma. Twende *hivi*.

109 Ni vigumu kwenye hizi, kupiga kona. Kanisa halitaki kuamini hilo, mnaona. Daima wanarejea nyuma kutoka kwenye msimamo wao wa kielimu. Hakika, hiyo ni shule, kivyake. Mnaona? Wanajifunza hayo kwa kusoma vitabu. Tunajua Hayo kwa ujuzi, wa kumwamini Mungu, mnaona, na kujua kwamba Yeye hufanya haya.

110 Ilikuwa ni kitendawili, kwamba Mungu aliifungua hiyo Bahari ya Chumvi na kufanya jambo hilo kuu.

111 Nuhu, katika wakati wake. Kumbukeni, Nuhu alihubiri katika ninii ya kielimu. . . katika ulimwengu wa kielimu kama tunaoninii . . . tunaohubiria sasa, siku ambayo walikuwa wameendelea sana katika sayansi kuliko tulivyo sasa. Kamwe tusingaliweza kujenga piramidi. Hakuna njia ya sisi kuijenga. Hatuna mitambo ya kuijenga. Baadhi yao—yao . . . Kama ulipata kuwa kule, mbona, hiyo—hiyo miamba ilikuwa na uzito wa tani nyingi, mamia ya tani, huko juu sana hewani. Hatuna mitambo ya kuinyanyua huko juu. Hatuna kitu kabisa cha kufanya hivyo, hamna nguvu zinazoweza kuinyanyua kule juu. Waliinyanyua.

112 Ninakumbuka shuleni, tulikuwa na mjadala juu ya hilo. Nilichukua u—upande wa kusema kwamba walikuwa na siri fulani. Hawakujua . . . Naye mpinzani wangu, alichukua upande wa kusema kwamba, mbona, waliwakusanya watu wa kutosha kuizunguka, nao wakafanya uwanja wenye u—usawa namna *hii*, kisha wakayafingirisha juu yake. Nikasema . . . Ni—nilikuwa nikifanya kazi kwenye kikosi cha kundi moja, nikasema, "Mbona, hatuwezi . . . Hebu chukua behewa lenye magurudumu, nayo yametiwa grisi, na kuyaweka kwenye njia ya reli, na huwezi kuweka watu wa kutosha pale kulisukuma behewa hilo, nalo ni tupu. Hiyo ni kweli. Unapata tu safu moja ya watu,

halafu mtu anayefuata ana—anamsukuma mtu huyo. Mnaona? Usingaliweza kulisukuma lisonge hata ufanye nini.

113 Walikuwa na siri. Walijua jinsi ya kufanya hivyo. Walikuwa na ninii kubwa zaidi, mtambo mkubwa zaidi. Piramidi hiyo iliwekwa kikamilifu sana katikati ya dunia, ikielekeza, hata hakuna ninii . . . Hamna—hamna kivuli kuizunguka, haidhuru jua liko upande gani. Kamwe haizungukwi na kivuli. Mnaona? Ni ninii—walifanya kitu kikamilifu. Nayo mitambo yao ilikuwa ni bora zaidi kuliko tuliyo nayo sasa.

114 Naye Nuhu alihubiri katika wakati huo mkuu wa kielimu. Naye Yesu akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu," wakati mwingine mkuu wa kielimu. Mnaona?

115 Sasa, kumbukeni, Nuhu alikuwa na ujumbe kutoka kwa Mungu, "Itanyesha." Vema, kamwe hakukuwapo . . . Mnaona, ulimwengu ulisimama wima siku hizo. Mnaona? Hawakuwa wamepata mvua. Lakini Nuhu akasema, "Itanyesha." Maji yalikuwa duniani, sio angani. Wangeweza kuchukua chombo na kuthibitisha hakukuwako na maji kule. Lakini Nuhu alisema, "Itatendeka, haidhuru." Mnaona? Nayo ikanyesha. Hicho kilikuwa ni kitendawili, mnaona, kitu ambacho kisingeweza kuelezewa. Bali Mungu aliitikisa-tikisa dunia, kwa kiwango ambacho ingeweza kunyesha. Kwa hiyo, mnaona, ilikuwa kitendawili kwa Nuhu kufanya hivyo.

116 Pia, ilikuwa ni kitendawili wakati Israeli waliposimama upande mmoja wa kilima, naye Goliathi upande mwingine wa kilima. Walikuwa na mpinzani mkubwa pale. Alikuwa ni mwanasayansi mkuu. A—alijua yote ndani na nje. Na wakati adui anapowazia amekufinyilia ukutani, hapo ndipo anapenda kubweka kwa sauti kubwa kuliko zote.

117 Nakumbuka, nilipoanza huduma hii kwa mara ya kwanza, loo, mchungaji huyo, Davis, aliniambia. Akasema, "Billy, kwani ulikula nini chakula cha jioni usiku ule?" Mnaona? Asingeweza kuelewa.

118 Nilikuwa na kundi la wahudumu pamoja nami. Wakasema, "Una shida gani? Unafikiri ya kwamba . . . "

Nikasema, "Sijali."

119 "Katika siku ya wakati huu wa kisayansi tunayoishi, nawe unataka kuniambia ya kwamba Mungu . . . "

120 Nikasema, "Sijali mnalosema. Mtu huyo, huyo Malaika wa Bwana, hajawahi kuniambia chochote kisicho kweli." Nikasema, "Kama akinituma huko nje, kutakuwako na mtu fulani atakayesikiliza. Kama kanisa la Baptisti halitaki kusikiliza, basi hii hapa kadi yangu ya ushirika." Hivyo tu. Nilijua Mungu alisema hivyo, na hilo lilitosha. Kweli.

Kasema, "Huwezi kufanya hivyo."

121 Hilo ni lile jitu limesimama huko, likisema, "Kama mtakuja huku, mnitumie mmoja wa watu wenu na kupigana nami, hapo hatutakuwa na umwagikaji wowote wa damu." Loo, jamani, ni rahisi vipi! Jinsi wanavyopenda kubweka wakati mambo yamekuwa hivyo. Kasema, "Acheni mmoja wa watu wenu aliye hodari sana . . . " Hakika, tangu mabega yake hata kichwani Sauli alikuwa mrefu kuliko jeshi lake, naye alijua vema kuliko kwenda kukabiliana na jamaa huyo kwenye maeneo yake.

122 Akasema, "Sasa, hatutamwua mtu yeyote. Tutaacha tu—tutaacha tu sisi wawili; mmoja wetu afe. Mtu mmoja tu afe badala ya majeshi yote hapa kufa." Alikuwa na ho—hoja ya kisaikolojia. Nanyi mnaona alisema . . .

123 Nao Israeli walitishika karibu kufa. Wasingetaka kukabiliana na changamoto hiyo.

124 Lakini siku moja maskini jamaa mmoja mwekundu akapanda kwenda kule, amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo mabegani mwake, ameinama, nywele zake usoni mwake, akapanda kuja pale kuwaletea ndugu zake keki za zabibu kavu, ambazo baba alimtuma kule. Jina lake lilikuwa ni Daudi; jamaa mfupi sana, mwembamba amesimama pale.

125 Lakini, unajua, kulikuwako, siku chache kabla ya hapo, nabii alikuwa amempaka mafuta.

126 Walitaka kuiweka juu ya kichwa cha kaka yake mkubwa, kwa kuwa alionekana mzuri zaidi, mwajua, aliyeleta picha nzuri mbele za wa—watu atakaosimama mbele zao. Anaonekana kama mfalme.

127 Loo, hilo ndilo ulimwengu ungali nalo, macho yao yamejaa Hollywood. Yanapaswa kujaa Kristo. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu ni vigumu sana kuwaletea watu utaratibu, Ujumbe. Wanataka kuwa Hollywood. Hollywood hung'aa. Vema, inang'aa. Sasa, ninaishi . . .

128 Mimi—mimi ni mtafutaji madini. Mwajua, dhahabu bandia hung'aa kuliko dhahabu halisi. Chochote kinachometameta, kila kitu kinachometameta si dhahabu. Hata hivyo, dhahabu haimetameti. Inameka.

129 Nayo Hollywood hung'aa kwa kumetameta, huku Injili humeka kwa unyenyekevu. Hollywood hung'aa kwa makanisa yake makubwa na mazuri, wahudumu wake wenye elimu, wa kisaikolojia wanaoweza kuzungumza na kutumia nomino zao na viwakilishi vyao na kila kitu sawa kabisa. Wakati, katika unyenyekevu, Injili ya Yesu Kristo humeka kwa utukufu wa Mungu. Ambapo, hawajui zaidi juu yake kuliko sungura angejua kuhusu viatu vya barafu. Wananinii tu . . . Ni umbali tu . . . Samahani tamshi hilo. Hapa sio mahali pa hilo. Mnaona? Na, ila hivyo ndivyo ni—ninavyojaribu kumaanisha, mwajua. Hawaninii, hawalielewi. Wanadhani linapaswa kupigwa msasa katika usomi. Na—nao watu wetu wa Kipentekoste wanafikia

hapo. Wahudumu wao hawana budi kwenda na kupata digrii nyingi za saikolojia, wajue jinsi ya kusema "amina" vizuri sana. Hiyo ni kweli. Loo, ni fedheha, enyi marafiki. Ni fedheha miongoni mwetu.

130 Sasa, sio kwamba ninalipinga kanisa. Ninapinga mfumo huo unaowachukua watu wanaomcha Mungu na kufanya hivyo. Haitubidi kung'aa. Kamwe hatutaweza kumleta adui upande wetu. Loo, kamwe hatuwezi kwenda upande wa adui na kujaribu kufurahia na kumetameta, tumevalia vizuri na tuna ukosi wa makasisi, na kila kitu, na kwaya yetu imevikwa majoho na kila kitu kama hao. Usiende kwenye maeneo yao. Hatuwezi kamwe kujilinganisha nao.

131 Waacheni, kama wana njaa, waje kwetu. Sisi ni wa Injili yote. Amina. Hebu na tukae hivyo. "Injili haikuja kwa Neno pekee, bali kwa nguvu na madhihirisho ya Neno." Hivyo ndivyo mwandishi alivyosema, "Nguvu na madhihirisho." Kwa maneno mengine, "Neno, lililothibitishwa, ndilo Injili," mnaona, Marko 16.

132 Angalieni sasa, tunaona ya kwamba katika siku za Nuhu, kwamba, wakati akihubiri, ilikuwa ni vigumu kwao kuamini kitu kama hicho. Wao . . . Nuhu kuamini kitu kama hicho. Lakini hatimaye kitendawili kikaja, na kikatendeka. Kweli ilinyesha.

133 Halafu katika siku za Daudi, tunaona ya kwamba wakati Sauli alipokuwa huko juu pamoja na jeshi lake lote kuu, na maskini jamaa huyu mwekundu akapanda kwenda kule, na—na akaja kumletea ndugu yake keki, kutoka kwa baba yake. Ndipo jitu hili likajitokeza na kujigamba mara moja zaidi kupita kiasi. Huyo hapo mtu wa Mungu aliyesikia majivuno hayo. Basi akageuka, akasema, "Mnataka kuniambia ya kwamba ninyi, majeshi ya Mungu aliye hai, mtamwacha Mfilisti huyo asiyetahiriwa, huko nje, asimame na kuwaambia siku za miujiza zimepita?" Ama, vema, kanuni ile ile, mnaona. "Kumwacha huyo mwanasayansi asiyetahiriwa kuwaambia, kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai?" Kasema, "Ninawaonea aibu, nanyi mnachukuliwa kuwa ni watu waliofunzwa." Kasema, "Nitaenda kupigana naye." Loo, ninavutiwa na ujasiri wake. Alijua alichoamini.

134 Kwa hiyo, Sauli akampeleka huko juu, kasema, "Mwanangu, sasa, navutiwa na ujasiri wako. Lakini, kumbuka, wewe si kitu ila kijana, unaona, naye ni askari wa vita tangu ujana wake. Unaona? Nawe hujui kitu kuhusu upanga na kadhalika. Sasa utaendaje kukabiliana na jamaa huyo, kukabiliana na changamoto yake?"

135 Akasema, "Sauli, nilikuwa nikichunga kondoo wa mtumishi wako, ndipo dubu akaja na kukamata mmoja wao. Naye akatoroka naye. Nilienda nikamnyang'anya. Simba aliingia na kukamata mmoja, nami nikamkimbiza. Nikachukua kombeo

na kumwangusha chini. Alipoamka, nikamwua." Akasema, "Bwana Mungu aliyenipa ushindi juu ya simba na dubu, ni zaidi sana vipi Yeye atanipa ushindi juu ya Mfilisti huyu asiyetahiriwa?"

136 Mwajua, ninawazia hayo ninapowaombea. Mnaona? Mnaona, simba anayeitwa "kansa" ameingia na kumkamata mmoja wa kondoo wake. Sina dawa yoyote. Sina sindano. Sijui radiamu ni kitu gani. Sijui chochote kuhusu theolojia na vitu hivi vya kujibunia. Ila ninajua Kombeo hili dogo ni kitu gani. Ninakuandama hapa sasa. Ninataka kukurudisha. Ni kondoo wa Baba yangu. Wakati mwingine sina budi kuwakemea, kuwakaripia, bali ni kwa sababu ninawapenda. Daima, daima, daima wekeni hili niani mwetu, kwamba upendo husahihisha.

137 Kama mvulana wako ameketi hapa nje barabarani, nawe useme, "Mwanangu, mpenzi, haikupasi kuketi hapo. Lakini nakutakia heri, kama ukitaka . . . " Huyo siye mama halisi wala baba. Utaenda umchukue na kuugeuza mkono wake, na kumpa maskini kichemsha tako. Ataninii—atamtengeneza kwelikweli, mnaona, kama ukimleta. Bali hutaketi pale chini, useme, "Sasa, mwanangu, mpenzi," wakati ukijua maskini jamaa huyo mdogo anaweza kuumia. Unampenda.

Hiyo ndiyo sababu ninakemea. Si kujaribu kuumiza dhehebu fulani. Ni, kumwamsha, "Hiyo ni Kweli."

138 Kwa hiyo tunaona ya kwamba Daudi alisema . . . Sauli alisema, "Vema, nakwambia, kama utaenda kupigana naye . . . " Akamvalisha silaha zake. Aha! Namwazia maskini Daudi, labda urefu wa futi tano, na mabega yaliyoinama; na kinga zake za mabegani zimechomoka *hivi*, na feleji hii. Sauli akaona . . .

139 Akasema, "Nivueni kitu hiki." Kasema, "Sijapata kukithibitisha hiki. Sijui kitu kuhusu maadili yenu na ninii yenu . . . tabia zenu zote za mimbarani na kadhalika mnazopaswa kuwa nazo." Mnaona? Alikuta kwamba fulana yake ya kikasisi haikumwenea mtu wa Mungu. Kwa hiyo akasema, "Nivueni kitu hiki. Sijui lolote kukihusu." Kasema, "Acheni niende na kile ninachojua kwamba ni Kweli, ambapo Mungu amenibariki." Hiyo ni kweli.

140 Acheni niende na Neno, sio na mpango fulani wa kielimu, ama kitu fulani ambacho mtu fulani amekipinda mahali fulani. Ninajua Neno la Mungu halitashindwa kamwe. Neno la watu wengine litashindwa. Naye Mungu Ndiye anayejifasiria. Kasema, "Hebu twende hivyo. Hebu tuliamini."

141 Daktari, hapana shaka, amekupa uchunguzi mzuri sana awezao, na akakusaidia kwa kila njia awezayo. Lakini hivyo ndivyo vema kuliko vyote ajuavyo. Tunajua jambo tofauti. Wakati matumaini yote yamekwisha, basi Yeye Ndiye ajaye kutusaidia.

142 Tunaona jambo hili, basi, Daudi, si kwa uta na mshale. Si kwa . . . Maana, usingeweza kulipiga lile jitu mahali popote. Alikuwa na mahali pamoja tu katikati ya macho yake.

143 Wazieni tu, mkuki wa—wa—wake mkubwa aliokuwa nao, mbona, labda ungekuwa na uzito wa ratili mia nne. Vidole vyake vilikuwa na urefu wa inchi kumi na nne. Pia wazia tu juu ya chapeo iliyokuwa juu ya kichwa chake, na deraya yake yote ya kifua.

144 Naye Daudi alikuwa na jiwe dogo. Hilo tu ndilo alilokuwa nalo. Alikuwa na mengine manne kwenye kombeo lake. Mnajua kile hayo mawe matano yalimaanisha? I-m-a-n-i katika J-e-s-u-s [Yesu—Mh.]. Hayo yalitosha. Mnaona? Alikuwa na imani, mnaona, imani, neema. Alikuwa ni neema ya Mungu. Ndipo akaenda kukabiliana na lile jitu. Alikuwa tu na mahali pamoja, Naye Mungu akalielekeza jiwe hilo.

145 Basi alipoliua jitu hilo, kuonyesha ya kwamba ingewezekana, ndipo majeshi wengine wakanyakua mapanga yao na wakatoroka. Walipigana nao hata mwisho.

146 Sasa, miaka michache iliyopita, walisema hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Lakini wakati tulipotoka nje tukathibitishe ulikuwako, basi moto uliwaka kwenye kanisa la Kipentekoste, nasi tumekuwa na uamsho wa miaka kumi na mitano. Ndugu, wale wakosoaji waliotaka kutoa dola elfu moja kwa thibitisho lolote, wame—wamenyamaza sasa, maana imethibitika. Taarifa za madaktari na kila kitu; kansa, vipofu, viziwi, bubu; hata kwa wale waliokufa, wamefufuliwa. Kwa sababu, unapokea tu imani, kwa kuona jambo moja likitendeka. Mungu yupo. Jambo lote limewekwa msingi juu ya hilo. Amini kila Neno alilosema; kwa ajili ya uponyaji. Ninaamini katika Unyakuo. Ninaamini katika kila kitu alichosema, kitatukia. Ilisababisha kitendawili, kitu ambacho kilikuwa si cha kisayansi, bali kilitukia, hata hivyo. Ilikuwa ni kitendawili.

147 Sasa, wazo langu lingine lilikuwa ni Samsoni, pamoja na taya lake la nyumbu. Ni ajabu, ajabu sana, kumwona jamaa huyu, Samsoni. Watu wengi wanajaribu kuwazia kwamba alikuwa—alikuwa ninii . . . Niliona matokeo ya kisaikolojia, ama picha ya Samsoni mwenye mabega makubwa kama mlango wa ghala. Vema, sasa, hilo li—lisingekuwa jambo la kigeni, kumwona mtu huyo akimnyanyua simba na kumrarua vipande-vipande. Bali Samsoni alikuwa maskini kibushuti kidogo sana, chenye nywele za kipilipili, kama tunavyoweza kumwita; maskini mbilikimo, kivulana cha mama, nywele ndefu za kipilipili zimening'inia mgongoni mwake. Basi unapoona . . .

148 Sasa, kumbukeni, simba alipokuja mbio, kumngurumia, angalia kilichotukia. Mnaona? Kulifanyika nini? Roho wa Bwana alikuja juu yake. Hilo ndilo lililoleta tofauti. Hiyo ndiyo sababu wangeweza kumfunga wakati mmoja wakati Roho wa Bwana

hakumjia; ishara yake ya Kinazarayo haikuwako. Lakini mradi tu angeihisi ishara hiyo ya Kinazarayo, acha chochote kije kitakacho kuja.

149 Na hivyo ndivyo ilivyo nanyi Wapentekoste. Mnapofikia kwenye sehemu hiyo ya maadili, mnapofikia mahali hapo ambapo mnataka kusikiliza kanuni ya imani na kadhalika namna hiyo, sijui habari zenu basi. Lakini kama mtairudia tu ishara hii ya Kinazarayo, Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani yako, kila kitu ni sawa basi. Usiogope chochote. Mradi tu Roho Mtakatifu yupo hapo apate kulitambulisha hilo Neno, acha waseme watakayo. Naam, bwana. Mungu angali anafanya kitendawili.

150 Nasi tunaona ya kwamba Samsoni, wazia hilo, akiwa na maskini taya la nyumbu lililo jepesi kuvunjika, ambalo lilikuwa limekaa huko nje uwandani kwa miaka mingi. Na mtu yeyote anajua ungeweza ukaligongesha kwenye mwamba, lingetawanyika vipandevipande. Naye. . . "Samsoni, Wafilisti wanakujia." Ndipo akaangalia kote. Hakuwa na kitu mkononi mwake. Nao hawa hapa Wafilisti elfu moja wamesimama pale. Kwa hiyo aliunyosha tu mkono, akaokota taya hili la kale la nyumbu.

151 Nanyi wazieni chapeo hizo, wakati mwingine zilikuwa na unene wa inchi moja na nusu, juu ya vichwa vyao. Naye akachukua hilo taya la nyumbu na kuwabwaga chini Wafilisti elfu moja. Aha! Hao wakitokeza kwenye miamba, wakijificha; kasema, "Mnataka kuonja baadhi yake? Teremkeni mje." Ilikuwa ni kitendawili. Lakini Roho wa Bwana alikuwa juu yake. Hilo ndilo lililoleta tofauti. Ilikuwa ni kitendawili kumwona mtu akiwa pamoja na watu wenye silaha nyingi, watu waliofunzwa kupigana, wakiwa na mikuki mirefu, na visu na kadhalika, chapeo na silaha, na mtu huyu mmoja amesimama peke yake huko kondeni ameshika taya la nyumbu, na kuwacharaza elfu moja wa hao. Bali ni kweli. Biblia ilisema ilikuwa ni kweli.

152 Mtu ambaye angeweza kung'oa malango ya Gaza, yenye uzito huko chini wa labda tani nane kila moja, malango makubwa ya shaba. Nao wakamzingira, usiku mmoja. Kasema, "Tutampata." Kasema, "Tutachambua kila unywele humu ndani mpaka tumpate, na tutampata." Lakini maskini kibushuti hiki kikajitokeza yapata usiku wa manane, kikaangalia huko nje, nayo malango yalikuwa yakimzuia. Kwa hiyo aliyang'oa tu na kuyaweka mabegani mwake, akapanda juu ya kilima na kuketi chini juu ya hayo. Ilikuwa ni kitendawili.

153 Huwezi ukamfungia Mungu ndani kwa uzio. Huwezi kumfungia popote. Yeye ni Mungu. Hakika. Ushindi mkuu alioshinda! Samsoni, Mungu alimtumia na kufanya kitendawili. Alimtumia mtu yeyote, mradi tu utalichukua Neno Lake, kama

umechaguliwa kwa Huduma hiyo. Endapo hujachaguliwa, vema, basi kaa tu na wale . . . Usikilize Ujumbe basi.

Sasa tutaharakisha. Naona nina yapata dakika kumi zilizosalia.

Kuzaliwa na bikira kulikuwa ni kitendawili.

154 [Mtu fulani anasema, "Unao muda hadi saa nne u nusu."—Mh.] Saa nne u nusu. Nitajaribu kutouchukua huo wote. Mmekuwa wasikilizaji wazuri sana, kila mahali. Nami na—na—najua ninapaswa kusimama hapa na kutoa hotuba kwa Wafanyabiashara hawa, na kadhalika, bali si—siwezi kutoa hotuba. Sijui lolote kuhusu hilo.

155 Ila tu, ninakumbuka hapa si muda mrefu uliopita, Billy, kabla tu ya wongofu wake, alikuwa pamoja nami. Ndipo akasema, "Baba." Tulikuwa mahali fulani, tukila. Kulikuwako na wimbo uliokuwa ukiendelea, mwajua, namna hiyo. Akasema, "Si ni wimbo mzuri huo?"

Nikasema, "Wimbo gani?"

156 Naye akasema, "Baba, unajua kuna jambo moja tu kukuhusu ambalo ni baya?"

Nami nikasema, "Ni lipi hilo, Billy?"

Akasema, "Jambo pekee unalowazia ni Kristo. Hamna lingine."

157 Nikasema, "Hiyo ni hongera, mwanangu." Naam, bwana. Alidhani angenikasirisha, mnaona. Lakini, hiyo, hiyo ni . . . Hiyo ilitosha. Ndivyo hivyo.

158 Ni—ni—ninamjua Yeye tu. Hivyo tu ndivyo ninavyotaka. "Na kumjua ni Uzima." Kujua mambo haya mengine siyajui, huenda—huenda yakamtambulisha kama mtu mwerevu. Nami sitaki kuwa mtu mwerevu; ninataka tu kumjua Yeye. "Namjua," kama vile Paulo alivyosema, "Katika nguvu za kufufuka Kwake, kusudi atakapoita nitatoka miongoni mwa wafu." Hivyo tu. Hivyo tu. Hivyo tu. Nami ninamtaka. Ninamtaka. Ninataka jina langu mahali pazuri.

159 Sasa, ilikuwa ni kitendawili wakati Mungu alipomfanya mwanamke kuchukua mimba. Ilikuwa ni kitendawili ambapo vile ambavyo Mungu, yule wa Milele anayeujaza wakati wote na Umilele, angeweza kushuka, awe maskini Mtoto mchanga akilia katika hori. Hicho kilikuwa ni kitendawili.

160 Ilikuwa ni kitendawili wakati alipokufa msalabani. Hiyo ilikuwa ni kitendawili, kuwazia kwamba Mungu angefanyika mwanadamu, ili aweze kufa kama mwanadamu, kuwakomboa viumbe Wake mwenyewe. Ilibidi afanye hivyo. Hakuna mtu mwingine. Kama huyo alikuwa mtu mwingine mbali na Mungu, mnaona, kama huyo alikuwa ni mtu mwingine yeyote mbali na Mungu, tumepotea.

161 Kwa mfano, vipi kama nilikuwa na mamlaka juu yenu kama vile Mungu alivyokuwa nayo juu ya kila kitu, nami ningesema, "Vema, hebu nitawaambieni, mtu yeyote anayeiangalia nuru *ile* atakufa, kama kuula ule mti"? Ndipo muda si muda wajua, ndugu huyu anayeketi *hapa*, huyu angeiangalia hiyo. Ninamsikitikia. Si—sitaki afe. Kwa hiyo nitamfanya Terry hapa, kuninii. . .Hilo lisingekuwa sawa. La. Vema, na kama ningemfanya mwanangu kumfia? Hilo lisingekuwa ni sawa. Kuna njia moja tu ninavyoweza kuwa mwenye haki, na hiyo ni kupachukua mahali pake.

162 Naye Mungu asingeweza kupachukua mahali pa mwanadamu, kwa kuwa Yeye ni Roho. Kwa hiyo Mungu aliumba seli ya Damu, ambayo ilikuwa ni Mwanawe Mwenyewe, Yesu Kristo. Ndipo Mungu akashuka na kuishi mle ndani, na akaishi, akajitambulisha Mwenyewe katika Kristo. Huyo alikuwa ni Mungu, Imanueli. Yesu alisema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anaishi ndani Yangu." Mnaona? "Mungu ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu." Yesu alikuwa ni mwili, maskani, Mungu alikuwa ni Roho iliyoishi ndani Yake.

163 Sasa, kwa mfano, tuna Roho kwa kipimo. Yeye alikuwa Nayo pasipo kipimo. Yeye alikuwa utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili, Uungu. Bali sisi tunayo kwa kipimo.

164 Sasa, kwa mfano, kama ile karama ndogo tuliyo nayo miongoni mwetu sasa. Sasa, hiyo ni kama kuchota kijiko kilichojaa cha maji kutoka baharini. Yesu alikuwa ni Bahari yote, bali hii ni kijiko kimoja tu. Ila kumbukeni, kemikali zile zile zilizo kwenye bahari nzima zimo kwenye kijiko hiki kimoja; ila tu kuna nyingi zaidi huko nje. Mnaona?

165 Yeye alikuwa ni Mungu. Sisi si Mungu. Sisi si Mungu. Ila, sote pamoja. . .Kama mkiangalia, limeonyeshwa, vizuri kabisa. Wakati ile Nguzo kuu ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli nyikani, ilipomtokea Mtakatifu Paulo. Wakati iliposhuka kwenye Siku ya Pentekoste, iligawanyika, na ndimi za Moto zikakaa juu ya kila mmoja wao. Ilikuwa ni Mungu katika Nguzo hii ya Moto, ile Logos, akijigawa Mwenyewe miongoni mwa watu Wake, ikionyesha ya kwamba Kristo na Bibi-arusi, mnaona, Mungu na kanisa Lake, wanafanyika mmoja. Mbona, ni kitu cha kupendeza kuliko vyote mlichopata kuona. Halafu, sote pamoja, ndugu; sio katika madhehebu mbalimbali, kamwe hatutasimama.

Mimi ni Mkentaki. "Pamoja twasimama, tukigawanyika tutaanguka."

166 Ni kwa nini Wahindi waliipoteza nchi hii kwa wazungu? Ni kwa sababu walikuwa—walikuwa wamegawanyika miongoni mwao.

167 Tutayapotezaje mashindano haya makuu? Ni kwa sababu tumegawanyika. Tutafanyaje jambo hilo? Inatupasa kukaa

pamoja. Sisi sote tunamwamini Mungu. Roho Mtakatifu anatuingiza sisi sote ndani. Itakuwa ni kitendawili kama Mungu akipata kutuunganisha, lakini atatuunganisha. Mwaminini tu. Kuzaliwa na bikira . . . Yeye anajua jinsi ya kutuma mateso ambayo yatatuleta pamoja. Sasa, kuzaliwa na bikira kulikuwa . . .

168 Sasa, Pentekoste ilikuwa ni kitendawili, jinsi ambavyo Mungu alichagua kundi la wavuvi wasio na elimu ambao hata hawakujua ABC za—zao. Inasemekana kwamba Petro hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe. Biblia ilisema ya kwamba yeye na Yohana, Matendo 4, walikuwa watu wasio na elimu wala maarifa, lakini hata hivyo walitambua kwamba walikuwa pamoja na Yesu. Hilo ndilo jambo muhimu. Na jinsi Mungu alivyochagua . . .

169 Sasa, ka—kanisa lilikuwa limelifunza kundi la watu kwa ajili ya hayo, maelfu ya makuhani hodari, wenye akili waliolijua hilo Neno, walisema, kutokana na maana zake zote, na kila kitu, walilisoma mchana na usiku, walikuwa nalo tu moyoni mwao, ila wakashindwa kuliona. Naye Mungu akachagua kundi la watu ambao hata hawakujua pale jinsi ya kuandika jina lao. Hiyo ilikuwa ni kitendawili. Kuacha kumchukua mtu ambaye alikuwa amefunzwa Neno, na kwa Neno; kisha kumchukua mtu asiyejua kitu kuhusu Neno, na kulithibitisha Neno kupitia huyo. Hicho kilikuwa ni kitendawili, hakika kilikuwa.

170 Ilikuwa ni kitendawili, jinsi ambavyo hao watu kwenye kile chumba cha juu pale, waliowaogopa Wayahudi, na walikuwa wametembea pamoja na Yesu, bali Roho Mtakatifu alipokuja, hawakuogopa tena. Hao wakaenda barabarani, wakipaza sauti, na kuanguka, na kufanya kama kundi la walevi. Hicho kilikuwa ni kitendawili. Roho Mtakatifu alikuja juu yao, wanawake na wote. Hawakuionea aibu Injili ya Yesu Kristo. Hakika ilikuwa ni kitendawili.

171 Maono ya manabii wa kale yalikuwa ni kitendawili. Hatuwezi kueleza ono. Utalielezaje ono? Ni kitu kinachompata mtu, kwamba anaona mambo kimbele miaka kadhaa ijayo. Linatendeka kikamilifu kabisa. Hilo haliwezi kuelezewa. Hakuna njia ya kisayansi ya kulielezea.

172 Hapa wakati fulani uliopita, katika—katika kubishana na daktari, nilipokuwa kwenye mkutano wa Kiwanis. Yeye alisema, "Bw. Branham, sitaki . . . Na—napenda kukusikiliza ukizungumza," akasema, "lakini—lakini, nakwambia," kasema, "si—siwezi kuamini chochote ila kilichothibitishwa kisayansi."

Nikasema, "Unadai kuwa Mkristo?"

Akasema, "Naam. Baadhi yake yananitatiza."

Nikasema, "Basi huwezi kuwa. Huna budi kuamini yote. Unaona?"

Akasema, “Si—siwezi kuamini kuzaliwa na bikira.”

173 Nami nikasema, “Vema, ninaweza kuamini—ninaweza kuamini kuzaliwa na bikira vizuri kuliko ninavyoweza kuamini kuzaliwa kwa kawaida.” Hakika naweza.

174 Vipi, kama kamwe ungeweza kuona kuzaliwa kwa kawaida, jinsi ambavyo hiyo mbegu ya kiume kutoka kwa mwanamume, na mwanamke. Na ambapo . . . Ni nani anayeamua itakavyokuwa? Hii hapa mbegu ya kiume kutoka kwa mwanamume, pamoja na he—hemoglobini, damu ndani yake. Na huyu hapa mwanamke, ambaye ni yai, hapa juu. Sasa, zile mbili za kwanza kukutana, hiyo mbegu inatambaa inaingia kwenye hilo yai, kisha hizo zingine zinakufa. Na kuna makumi ya maelfu mara maelfu ya hizo mbegu.

Nawe unasema, “Vema, ya kwanza inayotangulia.” La, la. Zinasimama.

175 Na huenda ikawa itakuwa ni mbegu itakayojitokeza kutoka katikati ya hizo mbegu, nalo yai litoke upande wa mwisho kabisa, nazo zitapitana na kukutana. Inaamuliwa kama itakuwa ni mvulana ama msichana, kama atakuwa na nywele nyekundu ama nywele nyeusi, atakuwa na tabia gani. Kitu Fulani, kisichojulikana na sayansi, huamua jambo hilo. Hicho si kitendawili, ni kitu gani? Hatua kwa hatua ndiyo njia ya karibu sana, tu—tunaelewa, bali sio wakati huo. Mungu huliamua. Mbona, kuzaliwa kwa kawaida, kama tungekuwa na wakati wa kuuchambua, hata kufikia kwenye kemikali ya damu na kadhalika, na kuthibitisha jambo hilo, jamani, ni siri kuu. Jinsi ambavyo tu—tunalichukua kikawaida!

176 Na hiyo ndiyo shida, sisi Wapentekoste, tunamchukua Mungu kikawaida sana. Jambo lote, tunaliachilia tu lipite. Msifanye hivyo. Hiyo si sawa. Msifanye hivyo. Liangalieni na kumsifu Mungu kwa ajili yake. Kila kitu kidogo kinachotukia, msifuni Mungu. Hilo ndilo analoonyesha, mnalithamini. Vipi kama mtu akiendelea kukufanyia mambo, hata huwashukuru, wala chochote kile, mnaona? Ndipo, baada ya kitambo kidogo, wanachoshwa na kufanya hivyo. Mnaona? Kwa hiyo, sasa, Mungu atachoka pia. Sasa, kumbukeni, Yeye anaweza kutoka kwenye mawe kumwinulia Ibrahimu watoto.

177 Sasa, hayo maono ya manabii wa kale hakika yalikuwa ni kitendawili. Hatuwezi kuyaeleza. Hayaelezeki, kuyafafanua, bali kila moja ya hayo lilitukia kulingana tu na vile walivyosema.

178 Sikilizeni. Sasa hivi, katikati yetu, Yesu Kristo yupo hapa. Hicho ni kitendawili, jinsi ambavyo Yeye yu hai baada ya miaka elfu mbili. Ni nani anayeweza kueleza hilo? Jinsi ambavyo Yeye, yule Roho, asiyeonekana, anavyoweza kuja miongoni mwetu, na kumchukua mtu fulani, na kujitambulisha Mwenyewe kikamilifu kabisa, ajiingize Mwenyewe ndani ya mtu

fulani; kama wewe, kama mwaminio, na kwa karama. Hicho ni kitendawili. Hakuna mtu anayeweza kuelewa hilo. Hakuna mtu anayeweza kujua. Jinsi ambavyo anaweza kumwambia kila mtu kikamilifu, ni kitu gani, na *hiki* ni nini, na *hiki* kiko wapi, na *kile* ni kitu gani, wala asikosee. Kwa sababu, Yeye ni Mungu. Hawezi kukosea. Hicho ni kitendawili.

179 Ikoje sasa? Nilipoingia jana usiku, na kumsikia ndugu yangu, meneja wangu wa huduma hapa, Bw. Borders, akizungumza (nilipata tu sehemu yake ya mwisho), kuhusu George J. Lacy akipiga picha ya yule Malaika wa Bwana. Ichunguzeni. Kama hiyo si Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli! Mnaona? Unajuaje? Ina tabia ile ile.

180 Wakati Yesu alipokuwa duniani, Yeye alisema, "Natoka kwa Mungu, Nami naenda kwa Mungu." Na sisi tunajua ya kwamba Yeye alikuwa MIMI NIKO. Naye MIMI NIKO alikuwa ile Logos, ile Nguzo ya Moto. Na ndipo wakati aliporudi kwa Mungu, na kupaa juu, Sauli wa Tarso alikuwa akienda zake Dameski, siku moja, na Nuru iyo hiyo ikashuka mbele zake, ikampofusha.

181 Sasa, angalieni, inawezekana kwamba mtu mmoja anaweza kuiona, na huyo mwingine hawezi. Makumi ya maelfu wameiona. Nilipokuwa nikisimulia habari Zake, walisema, "Loo, hiyo ni saikolojia. Aliwazia tu Hilo. Hao watu, wameshikwa tu na mhemuko."

182 Lakini wakati George J. Lacy alipoipiga hiyo picha, aliniambia siku hiyo, huko—huko Houston kule, je—jengoni, mbele ya hayo yote *Times*, *Life*, na *Collier's*, na yote hayo pale, magazeti. Yeye alisema, "Bw. Branham, mimi ni mmoja wa wakosoaji wako, pia." Akasema, "Bali nataka kukwambia. Nilisema ilikuwa ni saikolojia, lakini," kasema, "jicho la kimitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . muusia huyo amekufa." Mnaona? Akasema, "Lakini siku moja baada ya wewe kuondoka, itakuwa kwenye maduka ya malimali." Kasema, "Nina uwezo wa kujua hapajakuwapo na Kiumbe cha kimbinguni kilichopata kuthibitishwa kisayansi. Lakini," kasema, "Hiki kimethibitishwa kisayansi. Nuru iliipiga lenzi." Basi, mnaona, ule ushuhuda ambao nimetoa tangu nilipokuwa mvulana mdogo sana, kwamba nimeiona Nuru hiyo mbele zangu daima. Nanyi mwajua, mmesoma vitabu hivi na kuona matamshi yaliyothibitishwa. Mnaona? Ni kweli. Siko hapa kuwadanganya.

183 Ninaye mke. Nina mvulana mdogo, aliniita hivi majuzi usiku, kwa simu, akilia, "Baba, njoo nyumbani." Jinsi anavyolia na kuendelea, anaponiona nikiondoka, kwa sababu ya ajali nyingi sana katika ndege, na vitu kama hivyo. Wasichana wangu wadogo na kadhalika, mbona, hao ni wasichana wa baba. Mnaona?

184 Napokea mshahara kutoka kanisani mwangu. Sijapata kuchukua sadaka maishani mwangu. Siwaombi watu. Watu wanaponipa fedha, ninaziweka kwenye misheni za nchi za ng'ambo. Mnaona? Baadhi ya wadhamini wangu wameketi hapa sasa hivi, wanajua hiyo ni kweli. Situmii senti moja yake. Ninaipeleka Injili, mimi mwenyewe. Ninapokuwa na za kutosha mle, ninaondoka, nchi za ng'ambo, na kuwahubiria watu. Kwamba, kwamba ninyi—kwamba ninyi—ninyi . . . Mnawadhamini. Hawana hata hela moja ya pesa. Ndipo ninapoenda huko, basi ninaenda kule na kuihubiri Injili kule. Safari tayari imelipiwa na ninyi Wamarekani. Mnayajenga makazi yenu; hamjui lolote kuhusu hilo, lakini, Siku hiyo, mtaelewa. Mnaona? Ninyi ndio mnafanya hayo. Ninapata dola mia moja kwa juma kutoka kanisani mwangu, na hiyo ni kweli.

185 Sina sababu yoyote ya kuwa hapa nje, hakuna njia nyingine. Lakini ni—ni kitu fulani ndani yangu. Siwezi kukilaani wala kukibariki. Ni, ni, ni mdundo. Una—unanisukuma kwake. Mnafikiri ni rahisi, kusimama hapa na kuzungumza juu ya madhehebu, na kuwaona ndugu hawa wameketi hapa, ndugu ambao walizinyosha shingo zao moja kwa moja, wapate kunileta hapa?

186 Hata Wafanyabiashara wetu Wakristo, ndugu, wakati iliponibidi kumwambia Demos kuhusu, "BWANA ASEMA HIVI, kile kitakachotukia kwenye shirika hilo. Ambalo lilitukia, majuma machache yaliyopita, kwa Ndugu Ford na hao wengine. Nikawaambia, miaka miwili iliyopita, kuangalia kile kingetukia. Mnaona? Mnaliingiza kwenu, mtaliundia dhehebu. Hilo likitimia, basi nimemalizana nalo, dakika hiyo. Limekuwa ni oasisi, kwa sababu watu, wahudumu, wataingia, maana hapo ni mahali pao pa kuegemea. Mnaona? Ndipo ninafikia kuuleta Ujumbe na kupanda Mbegu, kila niwezacho.

187 Sio kwa sababu ninataka kuwa tofauti. Kama niko hivyo, basi mimi ni mnafiki. Basi, Mungu kamwe hatafanya mambo hayo kupitia mnafiki. Ati Mungu kumtambulisha mnafiki? Na iwe mbali na Mungu.

188 Haina budi iwe ni Kweli. Bali kama tungejitikisa tu kwa dakika moja na kutambua. Msifikiri ni mtu fulani. Mtu fulani hana chochote . . . wengine . . . Mungu hana budi kumchagua mtu fulani.

189 Sasa, ninyi wanahistoria hapa, hivi Mungu alipata kulitumia dhehebu? [Wengi wanasema, "La."—Mh.] Hasha. Sasa nataka kuwaulizeni jambo lingine. Mtu alipoinuka na ujumbe, na hilo shirika likajiundia dhehebu nyuma ya ujumbe huo, lilikufa papo hapo. Naye Mungu akaliweka kwenye rafu, nalo halikufufuka. ["Kweli."] Sasa hebu ulizeni tu, jiulizeni wenyewe swali hilo. Sasa, mnaona, hiyo si kuzungumza dhidi ya . . .

190 Sasa, kuna Wakatoliki. Watu wangu wote ni Wakatoliki. Mimi ni Mwairishi. Nao watu wangu wote ni Waairishi Wakatoliki, nao ni watu wazuri. Na mimi siwapingi Wakatoliki. Ni ule mfumo! Mimi siwapingi Wamethodisti. Siwapingi Wapentekoste. Ni mfumo huo unaotufungia nje. “Sisi ni wa *lile*,” mnaona, mnashughulikia ufanisi mmoja hapa. Nasi tunajaribu kumwonyesha Mungu wazi, Biblia. Nao tayari wameshaandika hati zao, utaratibu wa—wao wa dini, yale wanayoamini; na nje ya hayo, usingeweza kuvuka.

191 Nanyi mnafikiri ni rahisi kwangu kusimama hapa na kuwaambia hayo ndugu wanaonipenda? Mnafikiri ni rahisi kwangu kuwapigia ninyi dada makelele, wenye nywele fupi? Mnafikiri ni rahisi kwangu kuwapigia makelele ninyi wanaume, kwa kuwaruhusu wanawake wenu wavae kaptura na vitu kama hivyo; wakati wanawake hao wanachanga pesa, kuniunga mkono, umishenari, nchi za ng’ambo? Kama kusingekuwako na pesa zilizoingia kanisani, ningeweza...watoto wangu wasingeweza kuishi. Na mtu aliye mzuri kwako na mwema kwako, je! mnafikiri ni jambo rahisi kwangu kusimama pale, wakati ninawapenda watu?

192 Nilipokuwa mvulana mdogo, baba yangu akiwa ni mwuza pombe haramu, nilichukiwa. Mtu yeyote...Nikishuka kwenda mjini, nianze kuongea na mtu fulani, hakuna mtu angaliweza kuwa na uhusiano wowote nami. Hao, wangemwona mtu mwingine akija, wangaliweza kuzungumza naye, wangeondoka na kuniacha. Nami daima ni—niliwapenda watu.

193 Nilipokuwa mvulana mdogo niliketi, nikisoma kitabu cha—cha—changu cha historia. Nilikuwa nikisoma siku moja, na kuona mle ambapo Abraham Lincoln alishuka kwenye garimoshi hapa chini New Orleans. Nao walikuwa wakimpiga mnada mtumwa mkubwa mno mweusi kule chini, na—na wakamzalishe na wanawake wakubwa zaidi, wapate watumwa bora zaidi. Abraham Lincoln akavua kofia yake, na kutikisa ngumi yake. Alikuwa ni Mkentaki, pia. Akasema, “Hilo ni kosa. Hilo ni kosa.” Ningali nasema ni kosa. Mungu alimfanya mwanadamu. Mwanadamu akawafanya watumwa.

194 Mungu hufanya rangi yetu, kama tu vile anavyofanya maua. Ana ua jeupe, ua la bluu, ua jekundu. Achana nayo. Msiyachanganye mbegu. Yaacheni. Yaacheni jinsi yalivyo. Yote ni maua ya Mungu. Ni shada Lake la maua. Mungu alimfanya mwanadamu, naye mwanadamu akawafanya watumwa. Haitubidi kuwa watumwa.

195 Kama nilivyosema, huyu Martin Luther King anawaongoza watu wake kwenye kusulibishwa. Ni ukomunisti. Hakika, ndivyo ulivyo. Kama hao watu walikuwa watumwa, basi ningekuwa hapa chini nikiwapigania. Kweli. Lakini hao si watumwa. Ni ubishi, mahali wanapoenda shuleni ama

hawaendi. Hatutazungumzia hilo. Niliwazia tu ningelitaja. Mnaona? Vema. Tazama. Ni ibilisi tu. Hakika.

196 Sisi sote ni wanadamu. Sote tunatoka kwa Mungu. Mungu kwa damu moja aliyafanya mataifa yote. Mtu mweusi anaweza kunipa damu. Damu yake ni sawa tu na yangu. Yangu, ninaweza kumpa. Mimi ni nani kubishana? Yeye ni ndugu yangu.

197 Lakini siamini katika kufunga ndoa, ndoa za mseto namna hiyo. Siamini mzungu . . . Msichana mwafrika mdogo, mrembo, mwenye akili ana shughuli ga—gani kuolewa na mzungu, na kuzaa watoto machotara? Msichana mweusi mzuri, mwenye akili angetaka kufanya jambo kama hilo kwa sababu gani? Siwezi kuelewa hilo. Pia mwanamke mzungu angependaje kuolewa na mtu mweusi, apate watoto machotara? Kwa nini usikae jinsi Mungu alivyokuumba? "Ridhika na ulicho nacho." Mnaona?

Sasa angalieni kuzaliwa na bikira, na manabii. Vema.

198 Sasa, leo hii, Yeye angali hai. Angali hapa. Anajithibitisha Mwenyewe kwa Neno Lake. Neno hili ni Mungu. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Halafu Neno hili lilipangwa hapa kwa ajili ya siku hii, hapana budi pawe na mtu atakayekuja, kusudi Neno hilo liweze kuhuishwa na kulifanya Neno hilo hai.

199 Hiyo ni wakati Yeye alipozaliwa, kuzaliwa na bikira, lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida, na lisilo desturi. Mambo haya si desturi, na Yeye asingezuia.

200 Si zaidi ya vile Yusufu angaliweza kujiepusha kuwa alichokuwa. Hebu waangalieni wale wazee wetu wanne: Ibrahimu, Isaka, Yakobo, na Yusufu. Ibrahimu, kuitwa; Isaka, kuteuliwa; ama, vinginevyo. Ibrahimu, kuteuliwa; na Isaka, kuitwa; Yakobo, neema; Yusufu, ukamilifu, hamna neno dhidi yake. Huyo alikuwa ni Mungu, akifanya njia ya kutokea.

201 Kitu gani? Luther; Wesley; Pentekoste; jiwe la kufunika, wakati Kanisa na Neno vinakuwa sawa, kitu kile kile hasa, kikamilifu. Kila kitu katika hisabati katika Biblia, kinatuweka kikamilifu kabisa.

202 Laiti ningalikuwa na mwezi hapa pamoja na ninyi watu wazuri. Tungeketi na kulizungumzia hilo kabisa, na kuona. Mnaona? Tunaingia tu upesi na kutoka. Inaonekana ni mizuka kwenu. Mnaondoka na kusema, "Nashangaa," wengi wao. Sio ninyi, bali wengi wao, husema, "Nashangaa." Mnaona, inakubidi tu kugusia mwisho wake na kuondoka, ya kutosha tu muweze kuona. Mnaona? Na hivyo ndivyo Mungu anavyowaita watu Wake. Yeye daima huwaita hivyo. Angalieni sasa.

203 Sasa, Yeye angali hai leo hii, kitendawili, Nguzo ya Moto ikitambulishwa miongoni mwetu, kisayansi. Na ingali hapa, tangu huko nyuma kabisa nyikani pamoja na Musa. Yeye angali

ni MIMI NIKO. Sio "Nilikuwa," ama "Nitakuwa." MIMI NIKO, wakati uliopo, kisayansi. Na kwa ninii . . .

204 Angalieni Nguzo hii iliyoyapofusha macho ya Paulo, Sauli, na hao watu waliosimama pale hata hawakuona kitu juu Yake. Hawakuiona. Lakini ilikuwa angavu sana, kwa Paulo, ikampofusha macho. Daima alisumbuliwa na macho yake, tangu hapo na kuendelea. Mnaona? Yeye, waliiweka . . . Sasa, angalieni, huyo akiwa ni Mwebrania.

205 Naye akasema, "Bwana, U Nani Wewe?" Sasa, je! huyo Mwebrania angaliita namna fulani ya roho, "Bwana," mtu huyo hodari aliyefunzwa chini ya Gamalieli, mwalimu mashuhuri? Naye alijua sababu ya Yeye kuwa ni Bwana, ilikuwa ni Bwana aliyewaongoza watu Wake kutoka Misri. Kulikuwako na hiyo Nguzo ya Moto imesimama pale, ikisema, "Sauli, Sauli, kwa nini unaniudhi?"

Kasema, "Bwana, U Nani Wewe?"

Akasema, "Mimi ni Yesu."

206 Sasa hapa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mnaona? Alirudi, na akaahidi Hiyo kurudi katika siku za mwisho. Huyo hapo, Roho Mtakatifu, mnaona, akirudi katika siku za mwisho, kuwaleta watu. Sasa angalieni.

207 Moja kwa moja mwishoni mwa Myahudi na Msamaria, dhihirisho hili la Neno la Mungu, kujua mawazo yaliyo moyoni, Yeye aliwaonyesha hayo kabla hawajaondolewa. Na utaji juu ya uso wao (ambao nilitaka kuhubiri juu yake usiku wa leo) u—ulikuwa umewapofusha. Mnaona? Hawakuliona. Sasa, kama Yeye—kama Yeye alifanya hilo hapo awali, kwa hizo jamii mbili za watu . . . Ambazo, nasema kuna tatu: Hamu, Shemu, na Yafethi. Kama alifanya hivyo, na analiachilia kanisa hili hapa liingie kwa dhana za kielimu, basi alikosea. Lakini ni Yeye yule jana, kwa Hamu, Shemu; Yafethi, yeye yule; jana, leo, na hata milele. Naye aliahidi kufanya jambo hilo. Kwa hiyo Yeye hana upendeleo.

208 Basi angalia jinsi Ibrahimu alivyopitia kwenye ishara zake na kadhalika. Nayo ishara ya mwisho aliyoona ikifanywa na Mungu, ilikuwa ni Mungu Mwenyewe. Alimwona katika Nuru na kila kitu kingine; lakini Mungu Mwenyewe alidhihirishwa katika Mwanadamu aliyekula na kunywa.

209 Mtu fulani aliniambia wakati mmoja, mhudumu, Ndugu Foss. Akasema, "Ndugu Branham, unataka kuniambia, unawazia kwamba Yule aliyekula alikuwa, ya kwamba yule Mtu aliyesimama pale akila ndama huyo, na kula ugali, na maziwa, unafikiri kuwa huyo alikuwa ni Mungu?"

210 Nikasema, "Hakika. Ibrahimu alisema alikuwa. Yeye ndiye aliyezungumza Naye. Anapaswa kujua. Alisema alikuwa Elohimu." Nikasema, "Unaninii . . . "

211 Mnaona, alishuka kuja kufanya uchunguzi, kama vile alivyo sasa kwenye hukumu ya uchunguzi, aone waaminio ni akina nani. Tumekuwa tukipayuka-payuka sana kulihusu. Kuchunguza tu, aone waaminio ni akina nani hasa. Mnaona? Naye alijidhihirisha.

212 Yeye alituma maskini mfano wa ngano pale chini, kama katika jumbe za kisasa tunazosikia katika Babeli.

213 Lakini angalieni yale aliyofanya pale kwa hilo kanisa teule. Yeye alilipa nafasi, pia. Mnaona? Mnaona ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naye amenunua... Mungu wangu, Yeye alifanya nini? Mwajua, tumefanywa kwa elementi kumi na sita mbalimbali za dunia; chumvi, na—na petroli, na nurulimwengu, na kadhalika. Alinyosha mkono tu akachota konzi ya atomi, na nurulimwengu, petroli, kasema, "Whiu! Ingia ndani yake, Gabrieli." Ndipo akafanya mmoja apate kuingia ndani yake, Mwenyewe. Huyo ni Mungu wetu.

214 Basi alipompa Ibrahimu ujumbe Wake, alitoweka kisha akageuka moja kwa moja kuwa Mungu tena. Atomi hizo zote na kadhalika zikavunjika-vunjika tu. Kama vile moto unavyovunja asidi na—na kemikali katika mbao ama makaa, ama chochote kile unachochoma moto, kinarudia yasiyoonekana. Nina furaha sana Baba yangu yuko hivyo.

215 Mnaona, ninajua, baada ya mwili huu kuwa si kitu, wala huwezi kuona tena, ni kemikali tu mahali ulipokuwa; siku moja Yeye ataita, nami nitamjibu. Naam, bwana.

216 Mke wangu alisema, hapa si muda mrefu uliopita. Nilikuwa nikichana hizi nywele mbili ama tatu zilizosalia kwangu. Naye akasema, "Billy, unajua nini? Unakuwa kipara kabisa."

Nikasema, "Sijapoteza hata mmoja wa hizo."

Akasema, "Tafadhali, niambie mahali zilipo."

217 Nikasema, "Vema, kipenzi, nitakwambia, utakapofanya hivi: niambie mahali zilipokuwa kabla sijazipata; nitakubaliana nawe. Mnaona? Popote zilipokuwa kabla sijazipata, ziko pale zikiningojea niziendee." Amina. Haleluya!

218 Huyo Ndiye Mungu wangu. Huyo ni Mungu wetu. Hakika. Kama sisi ni watoto wa Ibrahimu, tunaamini hilo. Naam, bwana. Yeye ni Mungu wetu.

Sina budi kuharakisha.

219 Ile Nguzo ya Moto imetambulishwa kisayansi, na kwa matokeo, kwa tabia Yake na chochote kile, kwamba ni ile ile. Kama ilivyokuwa ilipokuwa ikiishi katika mwili wa Mwana wa pekee wa Mungu, ndivyo inavyoishi katika Mwili wa wanawe waliofanywa wana wenye mamlaka kwa ajili ya siku za mwisho.

220 Sasa, ninajua, ndugu, tumekuwa na huku kuiga kwingi. Lakini Biblia ilisema ingetukia, mwajua hilo, "Kama Yane na

Yambre walivyompinga Musa." Mnaona? Haina budi kutukia. Bali msiruhusu hilo—msiruhusu hilo liwapofushe. Mnapoona dola ya bandia, kumbukeni ilifanyizwa kwa iliyo halisi. Mnaona? Kama sivyo, ni—ni ya asili.

221 Lakini kuna Roho Mtakatifu wa asili, Kristo wa asili, hakika. Yeye ni Roho Mtakatifu. Angalieni sasa, nayo Nguzo ya Moto ingali hai leo, miongoni mwetu. Baada ya maelfu haya yote ya miaka, na ingali ipo hapa. Ni kitendawili.

222 Mbegu ardhini ni kitendawili. Nitafunga, yapata dakika kumi na mbili. Mbegu ardhini ni kitendawili. Jinsi ambavyo maskini mbegu hiyo itaingia ardhini na kufa. Halafu hiyo mbegu ndogo inapokufa ardhini, basi unaweza kuchukua konzi ya mavumbi na kuipeleka kwenye maabara na kuichunguza, usingeweza kuipata chembe hiyo ya uhai hata ufanyeje. Kisayansi hamna kitu mle, kinachoonyesha imo mle. Lakini acha tu jua lilenge pale mahali pake vizuri. Angalia kitakachotukia. Inatokea mahali fulani. Inaninii. . .Hicho ni kitendawili. Hawawezi kulielezea. Mnaona, kila kitu ndani yake kinakufa ila ule uhai, nao uhai hauonekani. Na popote ulipo maskini uhai huo, ni wa kimbinguni. Nao mwili wa kawaida umekwisha kabisa, bali wa kimbinguni ungali unaishi.

223 Sasa, maskini mbegu hiyo inaweza kuzikwa. Sasa nisikilizeni, enyi marafiki. Hiyo mbegu ndogo inaweza kuzikwa ardhini. Na endapo mbegu hiyo haijarutubishwa na mwenziwe, sijali mbegu hiyo ni ya kupendeza jinsi gani, haitaishi kamwe. Mnaona?

224 Sijali jinsi makanisa yetu yanavyokuwa ya kupendeza, jinsi tunavyojaribu kuvalia vizuri, jinsi tunavyokuwa wazuri na wenye akili, isipokuwa tukutanishwe na Mwenzi wetu (naye huyo Mwenzi ni Neno), mnaona, huwezi kufufuka. Hakuna njia ya wewe kufanya hivyo. Mnaona?

225 Mwajua, tunachukua mahindi. Tunaishi katika siku ya kuchanganya mbegu. Kila kitu ni chotara, mpaka hata wamelichanganyisha kanisa. Hiyo ni kweli. Wamelichanganya kanisa, kutoka kwa Neno, wakaliingiza kwenye kanuni ya imani ya kiakili, dhehebu. Kamwe Yesu hakusema, "Enendeni mkaunde madhehebu." Kamwe hakusema, "Enendeni mkajenge shule." Kasema, "Mkaihubiri Injili, mkadhihirishe nguvu za Neno la ahadi kwa ajili ya siku hiyo." Mnaona? Lakini tumelichanganya. Sasa tuna kanisa la kupendeza zaidi.

226 Enyi wanawake Wapentekoste, mama zenu walikuwa wakisimama pembeni, bila soksi; maskini viatu vizee, vilivyoraruka, hivyo viatu vya raba, wakipiga tari. Madhehebu yalimcheka na kumdhihaki. Baba alisimama pale, anapaswa kunyolewa, na anaokota mahindi barabarani mahali fulani, kuwalisha ninyi wototo. Ni vibaya sana mliachana na hayo.

227 Sasa, mna kundi la akina Riki mle ndani linalotaka kuja kama hao wengine, kama Israeli ilivyofanya, walitaka ninii—walitaka mfalme wao wenyewe. Mnataka kufanyiza wenu wenyewe. Mnaona? Na sasa mna nini? Kundi la akina Riki wenye elimu. Hiyo ni kweli. Wanaye huyu mwenye akili. Wanataka kuwa kama hao wengine, Dk. *Nanii wa nanii*, na Dk. *Nanii wa nanii*. Mnaona? Basi hilo limewafikisha wapi? Mnapendeza zaidi. Hiyo ni kweli. Ni makanisa mazuri zaidi. Lakini yuko wapi yule Roho aliyekuwa mle? Maombi ya mkesha yako wapi, "Hizo dhambi za mji"?

228 Kumbukeni, Roho Mtakatifu alisema, "Katika siku za mwisho, nendeni mkawatie muhuri wale tu wanaolia na kuomboleza kwa ajili ya machukizo yanayofanyika mjini."

229 Ninawatakeni ninyi wahudumu mweke mikono yenu juu ya huyo mshirika wa kanisa lenu, ninyi wahudumu Wapentekoste. Halafu, mtakapompata huyu, basi mje nami nitawaomba msamaha. Tafuteni huyo mshirika wenu asiyeweza kupumzika mchana na usiku, kwa ajili ya kulilia chukizo la dhambi zinazofanywa mjini. Asilimia tisini wao wanakaa nyumbani na kuangalia *Tunampenda Suzy*, badala yake. Loo, mnanena kwa lugha, hakika, mnaruka-ruka na kupaza sauti. Hiyo ni sawa, sina kitu dhidi ya hilo; wala sina kitu dhidi ya dhehebu lenu. Ila ninajaribu kuzungumza juu ya Uzima. Uko wapi?

230 Sasa nionyesheni mshirika huyo. Angalieni jinsi walivyo wa kilimwengu, wasiojali. Daima yaliyo nje huonyesha kilicho ndani. "Kwa matunda yao wanajulikana." Uko wapi? Nauliza tu. Jibu tu swali lako, kabla hujahukumu. Unaona? Uliza tu hilo swali. Sawa. Mnaona? Sijaribu kuwaudhi. Ninajaribu kuwasaidia. Mnaona? Ninajaribu kuwasaidia.

231 Mbegu hiyo haina budi kufa. Wakati Myahudi . . . Wayunani hawa walipomjia Yesu na kusema, "Tunataka kumwona Yesu." Yesu, Yeye alisema nini? Jambo la kwanza alilosema, "Punje ya ngano isipoanguka ardhini, ikafa, inakaa peke yake." Aliwaonyesha jinsi ya kumwona Yeye: kufa kwa nafsi yako, kufa kwa maadili yako, kanuni zako za imani, na yote haya. Zaliwa tu katika Neno, ndani ya Kristo. Hicho ni kitendawili, kukiona kikijitokeza. Naam.

232 Nakumbuka, hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa huko chini, mahali padogo panapoitwa Acton, Kentucky, huko nyuma kabisa milimani, sijapata kuwa huko hapo awali. Mimi na jamaa fulani, jina lake Bw. Wood . . . Yeye alikuwa ni Shahidi wa Yehova. Naye alikuwa katika mmoja wa mikutano, ndipo Roho Mtakatifu akanena. Alikuwa na mvulana aliyekuwa na mguu uliolemaa ukakunjamana chini yake namna *hiyo*. Nilikuwa nimesimama jukwaani, nikihubiri tu. Ndipo nikaangalia. Nikasema, "Ninamwona mtu ameketi huko nyuma kabisa jengoni." Refu mara tatu ya hili lilivyo hapa, hema

kubwa. Nami nikasema . . . Nasi tulikuwa huko karibu, loo, ni huko juu kwenye Maziwa Makuu. "Na—naye mtu huyu," nikasema, "Yeye ana mvulana. Mtu huyu anatoka Kentucky, huko chini kabisa Kentucky. Yeye ni kondrakta. Jina lake ni Banks Wood. Ana mvulana aliye na polio. Mguu wake umekunjamana chini yake." Nikasema, "BWANA ASEMA HIVI, ameponywa." Kwa hiyo, mwanamke huyo akasimama pale.

233 Sasa, kuna watu wengi tu wanaosimama papa hapa asubuhi ya leo, watu wangu, wanaomfahamu David Wood. Ni wangapi wanaomfahamu David Wood, wanaomfahamu? Hiyo ni kweli.

234 Papo hapo akasimama, na mguu wake ukanyoka kabisa. Hilo liliitatua shida ya Shahidi wa Yehova. Na mbali na hayo, kwa maono yayo hayo, amewaongoza watu wake wote.

235 Ndugu yake akaingia apate kumdhihaki na kumrarua-rarua kabisa, kasema, "Unafanya nini, kumfuata namna fulani ya mlokole kama huyo, baadhi ya haya madhehebu ya kisasa?" Msomaji katika Shahidi wa Yehova.

236 Akasema, "Vema, mtu huyo yuko huko nje akikata nyasi." Nilikuwa na maskini kofia kubwa ya manyasi, na huko nje uani, nikikata nyasi. Nikaingia, nikaketi chini. Akasema, Ndugu Banks akasema, "Huyu ni ndugu yangu, Lyle."

Nikasema, "U hali gani, Bw. Wood?"

Kasema, "Njema?" Loo, majivuno chungu nzima.

237 Nikaketi pale kidogo, ndipo Bwana akanipa ono. Nikasema, "Bw. Wood," nikasema, "Nadhani huamini hili?"

238 Akasema, "Hakika siamini." Kisha akasema, "Hakuna kitu kama mambo kama hayo." Kasema, "Ni mambo tu ya kubuni uliyo nayo kumfanya ndugu yangu achanganyikiwe."

239 Nikasema, "Unajua, Biblia ilisema, 'Neno moja dhidi ya Roho Mtakatifu halitasamehewa.'" Nikasema, "Ati nini? Na Yesu alikuwa akifanya jambo lile lile."

240 Mnaona, hakuwa ameliona bado. Mnaona? Kwa hiyo a—akasema, "Siamini kitu kama hicho."

241 Nikasema, "Vema. Kama ungeamini kitu kama hicho, ungemrudia mke wako ambaye umemwacha." Akageuka akaniangalia. Akaangalia kule. Sasa, hakujua ya kwamba nilikuwa nikishika mawazo yake.

242 Ni ajabu vipi, watu wanakuja huku, wanaona hayo jukwaani, na kuwazia kwamba hujui ilivyo hasa. Mbona, Yeye huyafunua mambo moja kwa moja karibu nawe. Mnaona? Lakini huwezi kuyasema. Yesu alijua Yuda alikuwa pamoja Naye wakati wote, lakini hata hivyo, mnaona, akaachana nalo, maana kuna kusudi lake. Mnaona? Na ninii tu . . .

243 Kwa hiyo, aliketi pale. Naye akasema . . . Akamgeukia Banks, kana kwamba Banks alimwambia. Huyo ni ndugu yake.

Nikasema, "Wewe una watoto wawili, wavulana wawili wadogo, wenye nywele za shaba." Akamwangalia Banks tena. Nikasema, "Unafikiria nini, kwamba Banks aliniambia hilo?" Nikasema, "Vipi kuhusu hili? Usiku wa juzi, ulikuwa ukiandamana na mwanamke mwenye nywele za kahawia, nanyi mlikuwa chumbani. Na katika chumba hiki, kuna mtu aliyebisha mlango, nawe ukamtuma mlangoni kwa kuwa uliogopa. Ni jambo zuri. Kichwa chako kingelipuliwa; mpenzi wake mwingine alikuwa amesimama pale na bastola mkononi mwake."

Akasema, "Mungu, nirehemu."

244 Mungu anajua vipi. Sasa yeye ni Mkristo mzuri, hodari. Baba yake alikuja vile vile, dada zake na hao wote.

245 Tulikuwa huko chini Kentucky, tukiwinda kuchakuro, katikati ya mmoja wa mikutano yangu. Nilikuwa na majuma mawili. Kukawa kukavu sana. Ni wangapi waliopata kuwinda kuchakuro? Loo, ndugu zangu, hakuna kitu kinachofanana nako. Kwa hiyo, hebu nipeni bunduki ya .22, katikati ya Agosti, nami niko nyumbani. Jinsi ambavyo Bwana hunena huko nje, na kujua mambo! Jinsi Yeye . . . loo, kadhalika. Angalieni. Hapo tulininii . . .

246 Kukawa kukavu kweli, huko vilimani tulikokuwa. Akasema, "Ninamfahamu mzee mmoja aliye kafiri." Kasema, "Yeye ana yapata ekari mia tano za vilima tu kama hivi, na huko mabondeni, vibondeni," tunaviita kule, "ambako unaweza kutembea, maana ni chepechepe." Kasema, "Huenda tukapata kuchakuro wachache." Kasema, "Bali ni jamaa mkali."

Nikasema, "Vema, hebu tushuke twende tukamwone."

247 Kwa hiyo yapata miezi michache kabla ya hapo, jinsi tulivyojua mahali hapo palikuwapo, nilikuwa na mkutano kwenye Uwanja wa Kambi wa Methodisti huko Acton, Kentucky. Ndipo usiku huo, wakati Roho Mtakatifu alipokuwa akifanya utambuzi, kulikuwako na mwanamke aliyeketi huko nyuma kabisa ya uwanja huo. Naye akaliita jina lake, na kusema, "Una dada anayekufa kwa kansa ya tumbo. Ndio kwanza atoke Louisville, nao walimfanyia upasuaji. Kansa ilikuwa imemwenea sana, hata ukaninii . . . Wasingeweza kumfanyia upasuaji. Naye ni Bibi *Fulani wa fulani*." Akasimama na kuanza kulia.

248 Nikasema, "Ulipoondoka nyumbani usiku wa leo, kwenye kabati ya marumaru ulichukua leso ndogo ukaiweka kwenye pochi yako. Ina alama ndogo, ya bluu nchani." Mnaona?

249 Mnasema, "Vipi? Hilo linasikika ninii sana . . . " Vema, vipi kuhusu Yesu akisema mahali alipokuwa yule samaki mwenye sarafu mdomoni mwake? Vipi kuhusu nabii akimwambia yule mtu kwamba nyumbu walikuwa wamerudi? Ninii tu, mnaona, unaninii tu . . . Ibilisi ana uigaji, naam. Bali kamwe husikii

kuhusu mmoja wao akiihubiri Injili na kuwaokoa watu, unaona, kwake. Unaona? Unaona? Inakupasa kujua vizuri zaidi.

250 Kwa hiyo basi tunaona, nikamwambia hivyo, kasema, "Chukua leso hiyo ukaiweke juu ya dada yako, kwa kuwa, BWANA ASEMA HIVI, ataishi."

251 Vema, sijui, je! yeyote wenu anamfahamu Ndugu Ben? Ninasahau jina lake la mwisho ni lipi. [Mtu fulani anasema, "Bryant."—Mh.] Bryant, hiyo ni kweli, Ben Bryant. Loo, jamani! Kamwe hamtaninii . . . Daima utamfahamu, ukipata kumwona mara moja. Kama angalikuwa hapa, angekuwa akipiga makele, akitupa mikono na miguu hewani namna hiyo, akipaza sauti. Kwa hiyo wakati mmoja . . .

252 Ndipo akaambatana na mwanamke huyu, kuiweka kwenye leso yake, na—na kuiweka leso hiyo juu yake kule juu.

253 Na yapata miaka miwili baadaye ndipo tulienda kuwinda kuchakuro. Akasema, "Hebu twende kule." Naam. Sikujua ilikuwa ni kwenye nchi ile ile. Ilikuwa yapata maili ishirini kutoka mahali tulipokuwa. Kwa hiyo tukateremka kule, kuelekea huko nyuma vilimani na kuteremka kwenye vibonde, na kupanda kwenye viwanja vya nyasi, na upande *huu*, mpaka tukatokea kwenye nyumba kubwa ya kale. Na hapo waliketi wazee wawili, wameketi chini ya mtofaa. Maskini kofia zao zilizoinama chini zimevutwa chini. Akasema, "Yule pale. Na, jamani, ni mkali sana." Kasema, "Yeye ni kisirani, kafiri."

254 Kwa hiyo, tukasimama. Nikasema, "Afadhali uende ukazungumze naye, basi. Yeye anajua mimi ni mhubiri, asingeturuhusu kuwinda hata kidogo." Kwa hiyo a—akasema . . . Akaenda pale na kusimama.

255 Alikuwa amesimama pale, tumbaku kubwa la kutafuna, mdomoni mwake, na limening'inia kwenye ndevu zake, amesimama pale. Kwa hiyo akageuka. Akasema, "Mbona," akasema, "aloo! Karibu."

256 Kwa hiyo, akafika pale. Ndipo akasema—akasema, "Jina langu ni Wood." Akasema, "Mimi ni Banks Wood." Kasema, "Ni- . . . tumekuwa . . . Mimi na rafiki yangu tumekuwa tukiwinda hapa," kasema, "kwa siku chache, hapa juu Acton," akasema. Kisha akasema, "Ni—ni . . . " Ama, "Ni kukavu sa—sana," kasema, "tusingeweza kuingia mwituni. Kuchakuro ni haba sana." Kasema, "Ninajua shamba lako limehadharishwa, lakini niliwazia labda nikija nikuombe, ungeniruhusu kuwinda."

Akasema, "Wewe ni Wood nani?"

257 Akasema, "Mimi ni mvulana wa Jim Wood." Huyo alikuwa ni Msomaji wa Yehova, Msomaji wa Shahidi. Mnaona?

258 Akasema, "Mzee Jim Wood ni mmoja wa watu waaminifu sana kule." Waliishi Indiana wakati huo. Kasema, "Mtu

mwaminifu sana aliyepata kuwako katika nchi hii." Kasema, "Hakika ninaweza kuamini hutaua mmoja wa ng'ombe wangu wala kuwasha moto." Akasema, "Jiweke huru." Kasema, "Nenda ukawinde humo." Kasema, "Nina ekari mia tano hapa. Jisikie nyumbani."

259 "Vema." Kasema, "Asante." Akasema, "Nadhani ni sawa mchungaji wangu aje pia."

Akasema, "Ati nani wako?"

Akasema, "Mchungaji wangu."

Je! ninachukua muda mrefu kupita kiasi? [Mtu fulani anasema, "La, bwana."—Mh.] Vema.

Akasema, "Mchungaji wangu."

260 Naye akasema, "Wood, usiniambie umekuwa duni sana hata inakubidi kubebana na mhubiri popote uendapo," akasema.

261 Nikawazia yaonekana wakati wangu wa kutokea umewadia basi, kwa hiyo nikatoka kwenye gari na kuzunguka-zunguka. Nikasema, "U hali gani?"

262 Akaniangalia, na kupangusa-pangusa tumbaku yake, mwajua, na kutema mate chini namna *ile*. Akasema, "Ati wewe ni mhubiri, en-he?" Nikasema . . . Akaangalia, nimejaa damu ya kuchakuro, na masharufu. Sikuwa nimeoga kwa majuma mawili, mwajua. Na—na kukaa mwituni, kulala, mwajua.

Na—na kwa hiyo nikasema, "Huenda nisionekane kama mmoja, lakini," nikasema, "ndivyo nilivyo."

263 Naye akasema, "Vema," akasema, "angalau ninaweza kukuheshimu kwa kuonekana kama mwanadamu." Akasema, "Huonekani kama wahubiri ninaoninii . . . "

Kwa hiyo nikasema, "Vema, asante, bwana."

Akasema, "Kwa namna fulani nawachukia ninyi jamaa."

Nikasema, "Ni—nilisikia, kutoka kwa Bw. Wood, unawachukia."

Akasema, "Unajua, mimi ni kafiri. Ndivyo ninavyodhaniwa."

264 Nami nikasema, "Naam, bali sidhani hilo ni jambo la kujivunia, sivyo?"

265 Naye akasema, "Vema," akasema, "Sijui." Akasema, "Nafikiri ninyi jamaa mnabwekea kichaka kingine." Nanyi mnajua maana ya hilo? "Mbwa mdanganyifu." Mnaona, 'kuuni hayuko huko juu. Mnaona? Kwa hiyo akasema, "Nafikiri mnabwekea kichaka kingine. Hakuna kitu kule juu, nanyi nyote mwasema uongo juu yake."

Nikasema, "'Hakika, hayo ni maoni yako."

266 Naye akasema, "Naam, nadhani hivyo ndivyo uanavyolidhania." Akasema, "Angalia hapa, bwana." Kasema,

"Unaona lile dohari la kale pale juu? Hapo ndipo ile nyumba ya kale ilipokuwa. Nilizaliwa pale juu. Babangu aliijenga nyumba hii hapa chini," akasema, "yapata miaka sabini na mitano iliyopita." Kasema, "Nililelewa papa hapa. Nimetembea kwenye milima hii. Nimeangalia kila mahali, juu angani, kila mahali. Sijapata kumwona Mungu yeyote, Malaika, wala chochote kile."

Nikasema, "Vema, hayo ni maoni yako."

267 Naye akasema, "Sijapata kumwona mmoja wenu ila yule niliyewazia alikuwa anasema uongo." Akasema, "Sitaki kukuudhi, bwana. Mimi . . . "

268 Vema, ni . . . Vema, niende kuwinda, ama nipambane naye? Kwa hiyo nikawazia nitampa tu . . . Mama daima alisema, "Mpe ng'ombe kamba ya kutosha, atajinyonga mwenyewe." Mnaona? Kwa hiyo, nikawazia, nenda tu.

Nikasema, "Naam, bwana. Hiyo ni kweli."

269 Akasema, "Ni—nilikutana . . . Nilisikia juu ya mhubiri mmoja wakati mmoja, ambaye, kama nikipata kukutana na jamaa huyo, nitazungumza naye." Kasema, "Huenda alikuwa na kitu fulani." Naye . . .

Tukazungumza kidogo, mwajua. Nami nikasema, "Ni nani huyo?"

270 Kasema, "Kulikuwako na jamaa mmoja . . . " Kasema, "Jina lake ni nani? Alikuwa huku juu Acton. Ninaamini walimwita . . . Nasahau jina lake lilikuwa nani. Branham."

Nikamwangalia Wood. Naye Ndugu Wood akasema, "En-he."

271 Akasema, "Wajua," kasema, "bikizee Casmo anaishi hapa juu ya kilima." Kisha akasema, "Tu—tulimpeleka kwa daktari huko Louisville, wakasema alikuwa na kansa. Nao wakamshona tu." Kasema, "Daktari aliwapa dawa wakampe, na kumtuliza mpaka atakapokufa. Naye huo ulikuwa ni karibu wakati wake wa kuaga dunia." Kasema, "Hata asingeweza kuamka kitandani." Kasema, "Ilitubidi kuvuta shuka aliyolalia. Yeye . . . Tusingeweza kumweka kwenye choo cha kitandani, mnaona, kilichokuwa chini yake hasa." Kasema, "Mimi na mke wangu tungeenda na kukisafisha kitanda chake, kila asubuhi."

272 Kisha kasema, "Kulikuwako na mhubiri kutoka huko mbali, mahali fulani katika Indiana-er." Kasema, "A—alishuka kuja huku, naye alikuwa na mkutano huko juu." Kasema, "Mtu huyo alisimama pale usiku ule na kumwambia dada yake, *Nanii wa nanii*, juu ya leso aliyokuwa nayo mfukoni mwake." Kasema, "Ukija kwenye . . . "

273 Kisha kasema, "Waliwaleta kundi la hao watakatifu wanaojifingirisha kule." Ndipo kasema, "Nilidhani walikuwa na Jeshi la Wokovu huko juu ya kilima usiku huo." Huyo alikuwa ni maskini Ben akilia jinsi hiyo, mwajua.

274 Kwa hiyo akasema—akasema, “Nikasema, ‘Vema, mwajua, alikufa.’ Kasema, ‘Hiyo ni familia yake.’”

275 Loo, mwajua jinsi ilivyo huko mashambani. Wanahudumiana, nao wanapendana na kushirikiana. Ni vibaya sana hatufanyi hivyo kwenye miji mikubwa.

276 “Kwa hiyo wao—walisema sisi . . . Nao walikuwa wakienda, kufa.” Basi akasema, “Nilidhani, ‘Vema, huyo ndiye.’ Kasema, ‘Vema, kumechelewa. Hatuwezi kuutoa mwili wake, mpaka asubuhi.’ Kasema, ‘Nitachukua mkokoteni wangu. Nitapanda niende kule nikamchukue, na kumtoa nje, tupate kumpeleka kwenye . . . huko Campbellsville, Kentucky, yapata maili arobaini kutoka kule, kwa mwenye kutayarisha mazishi.’ Kasema ilimbidi mwenye kutayarisha mazishi kuja kwenye barabara kuu, iliyo umbali wa kama maili nane, maili kumi, huko. Kasema, ‘Anaweza kuuchukua mwili wake kutoka hapo.’ Kasema, ‘Hakuna haja ya kwenda kule usiku wa leo. Watakuwa tu wakilia.’ Kasema, ‘Tutangojea tu mpaka mapambazuko.’”

277 Kasema, “Mwajua, kesho yake asubuhi nilipoenda huko, mwanamke huyo alikuwa amepika sambusa za matofaa, naye pamoja na mumewe wameketi mezani wakizila. Naye alikuwa akiishi kwa maji ya shayiri.”

278 (Niliwazia, “Loo-loo.”) Nikasema, “Loo, sasa, sasa, ngoja kidogo.” Nikasema, “Huamini hayo.”

Akasema, “Na wewe huamini hayo?”

279 Nami nikasema, . . . “Vema, wewe ndiye uliyesema hivyo.” Nikawazia, “Mzee, utanihubiria sasa, unaona.”

Akasema, “Kwani huamini?”

280 Nikasema, “Jamani, unataka kuniambia kwamba kitu kama hicho kingeweza kutukia katika nyakati hizi za kisayansi ambamo tuna daktari hodari sana?”

281 Akasema, “Kama huamini, nitakupeleka kule juu na kukuthibitishia.” Sasa kafiri ananihubiria kumhusu Mungu. Mnaona?

Nikasema, “Vema, wewe, kwani unamaanisha hilo?”

Akasema, “Naam.”

Nikasema, “Vema, ilikuwa nini?”

282 Akasema, “Ninataka kuninii . . . Kama nikipata kukutana na mtu huyo, nitamwuliza ni kitu gani kilichomwambia juu ya hilo, na jinsi alivyojua mwanamke huyo angepona. Mnaona?” Kasema, “Nitamwuliza juu ya hayo.”

283 Nikasema, “A-ha.” Nikasema, “Vema, hilo ni jambo zuri.” Kisha nikasema, “Aisee, naweza kula moja ya hayo matofaa?”

284 Nayo yalikuwa yametapakaa ardhini. Msimu wa kupukutika majani mwakani, mwajua, ilikuwa ni juma la pili la Agosti, nayo majani yalikuwa yakipukutika mtini. Nayo matofaa yalikuwako,

na yalikuwa ni matofaa mazuri. Nikaliokota na kulipangusa kwenye maskini suruali hizi chafu, nikaanza kulila, mwajua, namna hiyo.

285 Akasema, "Naam, karibu. Nyigu wanayala." Ni wangapi wanaojua nyigu ni nini? Kwa hiyo akasema, "Nyigu wanayala. Karibu."

286 Kwa hiyo nikasema, "Vema." Kwa hiyo, nikaanza kula. Nikasema, "Jamani, ni tofaa tamu."

287 Akasema, "Loo, ndiyo. Nilipanda mti huo hapo mimi mwenyewe, miaka hamsini iliyopita, karibu na ule mto." Nikasema, "Ala, wajua, majira ya majani kupukutika yatakuja mapema." Nikasema, "Hebu angalia pale." Nikasema, "Sijui ni kwa nini hayo majani yanaanguka kutoka kwenye ule mti kabla hata hatujapata usiku wenye baridi? Agosti, joto zaidi."

"Loo," akasema, "uhai umeuacha."

"Loo, ndio unaofanya hivyo?"

Akasema, "Naam, yanapauka na kuanguka."

Nikasema, "Uhai huo ulienda wapi?"

Akasema, "Ulishuka ukaingia kwenye mzizi."

Nikasema, "Vema, kwa nini ufanye hivyo?" Mnaona?

288 Akasema, "Vema, ni kwa sababu usipofanya hivyo, usiposhuka uingie kwenye mzizi," akasema, "baridi kali itauua mti huo. Chembe ya uhai imo kwenye ninii—kwenye ninii—utomvu ulio katika mti huo, nao unaingia kwenye mzizi." Basi ni ushuhuda mzuri jinsi gani pale, mnaona, wa mauti, kuzikwa, na kufufuka, tena. Mnaona?

Nikasema, "Basi, inakuwaje basi? Unakaa kule chini?"

Kasema, "La, la."

289 Nikasema, "Hurudi kwenye majira mengine ya kuchipua na kukuletea kichala kingine cha matofaa."

"Naam."

"Nawe unaketi hapa na kuyala."

"Naam."

"Halafu unasema ati hujapata kumwona Mungu."

Akasema, "Vema, hayo ni maumbile tu."

Nikasema, "Kweli?"

"Naam, bwana."

290 Nikasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani. Kama ni maumbile tu, niambie ni akili gani inayouonya mti huo, utomvu huo mtini? Hauna akili yake wenyewe. Lakini ni akili gani inayoutelemsha utomvu huo mzizini, kasema, 'Shuka hapa chini ukajifiche kwenye kilindi cha ardhi sasa, hata shida zote zitakapopita, kisha nitakurudisha juu tena'? Unaona? Niambie.

Uhai uliokuwamo kwenye jani, ni mwili tu uliokufa. Jani hilo likaanguka. Uhai wenyewe ukateremka, kisha ukarudi na jani jipya. Unaona?" Nikasema, "Uhai ulijificha, ukaingia ardhini."

291 Ayubu, kama nilivyosema jana usiku, "Loo, nifiche kaburini, unaona, hata ghadhabu Zako zitakapopita." Aliona dhiki ikija, hakika. Mnaona? Angalieni, yeye alisema, "Nifiche."

Akasema, "Vema, hayo ni maumbile tu."

292 Nami nikasema, "Bwana," nikasema, "kama nikiweka ndoo ya maji hapa nje juu ya nguzo, na kisha kila Agosti maji hayo yateremke chini ya nguzo, halafu kwenye majira ya kuchipuka mwakani yapande yarudi kwenye ndoo tena?"

Akasema, "Loo, loo, la. Hayana uhai wowote."

293 Nikasema, "Haya basi. Sasa umelipata. Unaona, ni uhai." Nikasema, "Unaona, huo ni Mungu."

Akasema, "Unajua, kamwe sikuwazia hilo."

Nikasema, "Waweza kuniambia ni kitu gani kinachofanya hivyo?"

294 Akasema, "Sijui. Sijui ni kitu gani kinachofanya hivyo. Nikasema, 'Ni maumbile.'"

Nikasema, "Vema, ni Nani anayetawala maumbile? Je! maumbile ni akili? La."

Akasema, "Vema, kamwe sikuwa nimeliwazia jinsi hiyo hasa."

295 Nikasema, "Nitakwambia, ninatoka niende hapa nje, kuwinda kuchakuro, kama ni sawa."

Kasema, "Karibu."

296 Nikasema, "Nitakaporudi, nitakaporudi . . . Wewe chunguza kwa makini sana sasa. Ndipo nitakaporudi, uniambie ni Akili gani inayouambia uhai huo katika mti huo kuteremka kuingia kwenye mzizi kisha urudi kwenye majira ya kuchipua, nami nitakwambia Nini, Kitu kile kile kilichoniambia mwanamke huyo ataishi kule juu, aliyekuwa na kansa."

Kasema, "Ati alikwambia?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Wewe ndiwe yule mhubiri?"

Nikasema, "Naam, bwana. Mimi ni Ndugu Branham."

297 Na hapo chini ya mti huo, alasiri hiyo, kwa kitu kidogo rahisi kama hicho, nikamwongoza kwa Kristo, machozi yakitiririka mashavuni mwake.

298 Mwaka mmoja baadaye, nikashuka kule. Nikaegesha gari langu uani. Walikuwa wamehama. Alikuwa ameondoka. Alikuwa amekufa. Basi niliporudi, yule mama alikuwa amesimama pale, apate kunikemea vikali, kwa kuwinda kwenye

shamba lenye marufuku. Yeye alikuwa ameniambia, niwinde wakati wowote niliotaka kuwinda. Yeye hakuwa . . . hakumsikia akisema hivyo.

299 Kwa hiyo nikaja, nikasema, "Sa—samahani." Kasema, "Nilikuja hapa mapema asubuhi ya leo, nikaegesha gari hapa mahali ungeweza kuliona."

Kasema, "Zile leseni za Indiana pale?"

Nikasema, "Naam, mama." Nikasema, "Mumeo . . . "

300 Kasema, "Mume wangu amekufa karibu mwaka mmoja." Alikuwa ameketi, akimenya matofaa kwenye ua wa nyuma, kutoka kwenye mti ule ule. Nikasema, "Vema, aliniambia kabla hajafa."

Kasema, "Siamini hilo."

301 Nikasema, "Nilikuwa nimeketi pale pale nje siku moja." Kisha nikasema, "Nikaja na nilikuwa nikizungumza naye. Walisema alikuwa kafiri."

302 Akaangusha tofaa hilo na akageuka kuniangalia. Kasema, "Je! wewe ni Ndugu Branham?"

Nikasema, "Naam, mama."

303 Akasema, "Nisamehe." Akasema, "Nisamehe." Akasema, "Yeye alikufa, akipaza sauti, mikono yote miwili hewani, akimsifu Mungu; akijua, kama vile lile jani linavyorudi, yeye angerudi tena."

Mnaona, kitendawili, hakielezeki.

304 Akiwa ameketi, akila aiskrimu, ninii tu . . . (Ninafunga.) Akiwa ameketi, akila aiskrimu, si muda mrefu uliopita. Mzee mmoja mwuza dawa aliniambia, kasema, "Unajua, Ndugu Branham, nina ninii . . . Unaamini katika kitendawili?"

Ndipo nikasema, "Naam."

305 Kasema, "Nilisikia ujumbe wako wakati mmoja kwenye kanda, '*Kitendawili.*'" Akasema, "Miaka mingi iliyopita, wakati wa kuzorota kwa uchumi," kasema, "watu wilayani, walioishi kwa msaada, iliwabidi waje wapate hundi," na kusema, "ya kupata dawa zao." Kisha kasema, "Iliwabidi kufanya milolongo mirefu." Kisha kasema, "Siku moja, jambo la ajabu." Akasema, "Nilikuwa nimeketi hapa nyuma nikisoma gazeti, naye mvulana wangu mdogo," kasema, "alikuwa huko juu."

306 Kisha akasema, "Maskini mwanamke mmoja alikuwa amesimama mstarini huko nje. Alikuwa karibu kujifungua, wajua, wakati wowote. Ilimbidi kupata dawa. Daktari aliziagiza. Ilimbidi ajaziwe maagizo hayo." Kwa hiyo, kasema, "Mvulana huyo . . . Mama huyo asingeweza kusimama muda mrefu zaidi. Akamleta pale juu. Kasema, 'Bwana, nitasimama mstarini. Sina budi kumpeleka mke wangu nyumbani.' Mnaona? Kasema, 'Naweza kumpeleka nyumbani? Daktari alisema

tuwe na dawa hizi alasiri ya leo, bali asingeweza kusimama muda mrefu zaidi.' Kasema, "Naweza—naweza kujaziwa maagizo haya? Unaona, nina hundi hapa. Sina budi kupata tu muhtasari wa kusema ninaweza kufanya hivyo.' Kisha kasema, 'Nitairudisha moja kwa moja kwako.'

307 "Basi yule mvulana mdogo, hakika, katika wakati wa kuzorota kwa uchumi, mwajua, akasema, 'Sa—samahani.' Kasema, 'Si—siwezi kufanya hivyo.' Kasema, 'Tu—tuna amri ya kutofanya hivyo.' Kasema, 'Siwezi kufanya hivyo.'"

308 Ndipo kasema ilitokea kwamba aligeuka tu na kusikiliza ilivyokuwa. Akaangalia pale juu. Naye maskini mwanamke huyo mdogo, mdomo wake ukiwa mweupe, huku anajishikilia ukutani, namna *hiyo*. Naye mume wake amesimama pale, mzuri tu awezavyo kuwa. Akasema, "Ngoja kidogo, mwanangu."

309 Kasema, "Nilienda nikachukua hayo maagizo, nikayajaza, nikayarudisha." Kasema, "Ndugu Branham, nilipoenda kuyatoa," akasema, "Niliangalia. Niliyaweka mikononi mwa Bwana Yesu." Akasema, "Nikayapangusa macho yangu. Nikaangalia tena." Kasema, "Yeye Ndiye aliyeunyosha mkono na kuyachukua maagizo hayo." Kasema, "Je! unafikiri nimejisahau, Ndugu Branham?"

310 Nikasema, "La, la. 'Kadiri mlivyowatendea walio wadogo katika watoto Wangu hawa wadogo, mmenitendea Mimi.' Kitendawili, hakika, kilikuwa ndicho. Kililitimiza Neno."

311 Kuna vitendawili vingi, vikubwa tungeweza kuvizungumzia. Lakini, marafiki wapendwa, tunapofunga, hebu tuwazie jambo hili. Kuna kimoja kikubwa kinachokuja, Unyakuo. Hebu sote tuwe tayari kwa ajili ya hicho pale. Hebu tuziweke tayari nafsi zetu sasa mbele za Mungu, kusudi wakati huo ujapo, tupate kwenda.

> Baragumu Yake Bwana wakati ikipigwa, na hapatakuwapo na wakati tena,
> Ile asubuhi ipambazuke Milele, angavu na nzuri;
> Na wakati watu wetu waliochaguliwa watakapokusanyika Nyumbani mwao ng'ambo ya anga,
> Majina yaitwapo huko ng'ambo, sote na tuweko.

312 Niliketi hapa mezani asubuhi ya leo, nikiwaangalia. Mwajua, huenda tusile kiamshakinywa kingine pamoja. Mwajua hilo? Huenda huu ukawa ndio wakati wa mwisho tutakaokula kiamshakinywa pamoja. Bali lipo jambo moja la hakika, kwa neema ya Mungu, tutakuwa kwenye chakula cha jioni pamoja, moja ya siku hizi. Nitaangalia upande wa pili wa meza na kuwaona. Nitasema, "Je! mnakumbuka wakati tulipokuwa huko Tampa?"

"Naam. Hapo—hapo ndipo nilipojisalimisha kikamilifu." Jamani!

313 Hakika, machozi yatatiririka mashavuni mwetu. Ndipo Mfalme atajitokeza, uzuri Wake, ayapanguse machozi yote kutoka machoni mwetu, aseme, "Msilie tena, watoto. Yote yamekwisha. Ingieni katika raha za Bwana, mlizowekewa tayari tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu."

Na tuinamishe vichwa vyetu.

314 Baba wa Mbinguni, muda wa wakati wetu unamaanisha mengi sana, Bwana. Sisi ni wa duniani tu. Na dakika chache tu hapa na pale, nao unatuishia. Na tunapozungumza na Wewe, tunaamini ya kwamba tumefufuliwa pamoja Nawe sasa, "tumeketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu." Nawe uko pamoja nasi asubuhi ya leo. Tunafahamu hilo. Tunajua ya kwamba Wewe upo hapa.

315 Nasi tunazungumza juu ya somo la kitendawili. Hicho ni cha kimbinguni. Ni kitendawili kwamba Wewe ulipata kumwokoa mwovu kama mimi. Jinsi ambavyo watu wangu wote, wenye dhambi, walilelewa, huko misituni, gugu, ulipataje kufanya punje ya ngano kutoka kwake, Bwana? Kitendawili. Karibu watu wangu wote wakifa huku wamevaa buti zao, wakipigana, bunduki. Ee Mungu! Lakini neema Yako iliniokoa. Daima nashukuru, Mungu. Daima nashukuru.

316 Na—nawaombea wengine, Bwana. Kama ningeweza... Kama wangaliweza tu kumjua Mtu huyu wa ajabu, Kristo. Nami ninawaona, Bwana, wameketi wakiwa na dhana zake za kielimu, na kweli hawajui Mtu huyo, Kristo, ni nani. Bwana, lifanye halisi kwao.

317 Wasaidie hawa, kundi hili zuri la watu, Bwana, ndugu zangu. Wahudumu hawa na wafanyabiashara ambao, katika saa hii kuu ya giza, wamejitambulisha wenyewe, Bwana, imani zao. Hata wakati mwingine dhidi ya mawazo bora ya madhehebu yao, wanalitaka haidhuru. Wabariki, Baba. Mbariki kila mmoja.

318 Sasa, wakati tumeviinamisha vichwa vyetu. Sijui, asubuhi ya leo, kama kuna yeyote hapa asiye na hakika kwamba lile jani dogo, ambalo unamfanyia mtu mwingine uvuli, kama uhai ungeliacha, kurudi ardhini, je! lingeishi tena? Je! mbegu hiyo imerutubishwa na Mwenziwe, ambalo lingelifanya kurudi? Kama huna hakika kabisa nalo, rafiki, hebu tuliombee sasa.

319 Unajua huo Uhai ni nini? Ni Roho Mtakatifu. Endapo hujampokea huyo Roho Mtakatifu ndani yako, ambaye Ndiye Uhai uliokuwamo kwenye ule Mmea wa kwanza uliofufuka, unaona, Kristo, malimbuko ya wale waliolala mauti. Sasa, endapo ule Uhai uliokuwa ndani Yake, Roho yule yule, hayumo ndani yako, haidhuru unajaribu kuwa mzuri vipi, huwezi kufufuka. Hamna kitu mle cha kukufufua. Unaweza kuchukua mahindi, uyachanganye na kitu kingine, hayatazaa

tena. Yamekwisha. Kama wewe ni mfuasi tu wa kanisa, na wewe kweli hujajazwa na Roho wa Mungu.

320 Ninajua ni vigumu kuchukua msimamo sasa, maana wanakuita kila kitu. Hilo halijalishi. Walimwita kitu kile kile. "Nao wote wanaoishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu watateswa." "Waliwatesa manabii waliowatangulia." Wanafanya hivyo leo hii. "Waliwatesa wale waliowaamini manabii waliowatangulia, vivyo hivyo nanyi watawatesa."

321 Kama huna hakika yake, huku kichwa chako kimeinamishwa na macho yako yamefumbwa, nitakuomba ufanye jambo moja zaidi. Naomba unielewe. Inamisha moyo wako, sivyo? Inamisha tu moyo wako kwa dakika moja. Ndipo useme, "Ndugu Branham. . . " Hakuna mtu anayeangalia ila mimi na Mungu. "Mimi—mimi, kwa kweli, nina shaka kidogo kama nitafufuka tena. Utanikumbuka kwa maombi?" Sasa, hatuwezi kufanya wito wa madhabahuni, zaidi ya wewe kuinua tu mkono wako. Inua tu mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham." Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe, wewe, wewe. Naam, kila mahali. Asante Mungu. Asante.

322 Baba wa Mbinguni, maneno madogo, rahisi, bali hata hivyo Roho Mtakatifu aliye mkuu yuko karibu, Yeye ajuaye siri ya moyo. Nao wameinua mikono yao kwamba hawana hakika kulihusu. Lakini, hata hivyo, wa—wa—wanakuamini. Hao, wanataka kukuamini. Nao wana—wananinii tu . . . Hawana Huo. Hawajui jinsi barabara hiyo itakavyokuwa, kuteremka kwenye tawi; kutoka kwenye tagaa, kuingia kwenye tawi; kutoka kwenye tawi, kuingia shinani, kurudi juu tena.

323 Wewe Ndiwe Kiongozi, Bwana. Kama vile kwenye ziara ya mawindoni, usipopiga simu mapema na kufanya matayarisho upate kiongozi, unaweza kupotea. Nasi tunapiga simu mapema sasa kwa Kiongozi wa Uzima ambaye alisema, "Mimi Ndimi ufufuo na Uzima." Unaijua njia, Bwana. Ninakuandikia barua hii ndogo, kwa njia ya maombi. Nao wanaandika kitu kile kile. Wapokee, Bwana.

324 Wanataka kushika nafasi kwa ajili ya Unyakuo, kile kitendawili kikuu. Wamekuwa mkutanoni juma hili, nao wameona Uwepo Wako, na wanajua Wewe upo hapa. Si wagumu jinsi hiyo, kuwazia ya kwamba . . . Watu wanaozileta Jumbe si Malaika; ni wanadamu. Nasi tunajua ya kwamba Wewe hutenda kazi kupitia wanadamu. Nami naomba ya kwamba nafasi zao zitawekwa asubuhi ya leo. Ulisema, "Yeye atakayenikiri mbele za wanadamu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu." Siku hiyo itakapowadia, basi Wewe utawaongoza kuvuka mto; kutoka kwenye tawi, kushuka kwenye shina, kuingia kwenye mzizi wa mti, kama Wewe ukikawia; basi uwarudishe juu tena, kwenye kile kitendawili kikuu mwishoni mwa safari. Ni Wako, Bwana. Ni kati Yako na wao.

325 Ninaomba, Bwana, kama hawajapata kubatizwa kwa ubatizo wa Kikristo, kwamba watafanya hivyo. Ndipo watajazwa na Roho Mtakatifu, Uhai utakaowaongoza. Kwa kuwa ni katika Jina la Yesu Kristo tunaomba hili. Amina.

326 Asanteni, kwa wema wenu, tumepitiliza sana. Nami ninajisikia kwamba ninawajibika. Kama kuna cha zaidi kitakacholipwa kwa ajili ya ukumbi mbali na ilivyokuwa asubuhi ya leo, nitakilipia mimi mwenyewe. Tutaliweka sawa.

> Nampenda (Yeye!), nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> . . . Kalvari.

327 Angalieni utaratibu wa Unyakuo, jinsi utakavyokuwa. Tutakutana sisi kwa sisi kabla hatujakutana Naye, maana, Yeye alijua ya kwamba tutakapofika kule, nitakuwa nikishangaa kama ulikuwa pale, nawe unashangaa kama nilikuwa pale. "Lakini," Biblia ilisema, "sisi tulio hai na tuliosalia hata Kuja kwa Bwana hatutawatangulia, ama kuwazuia wale waliolala mauti. Kwa maana parapanda italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza, kisha sisi tulio hai na tuliosalia tutabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua, kisha tutanyakuliwa pamoja nao." Loo, itakuwa ni ibada ya jinsi gani wakati huo. Sasa, "Kunyakuliwa pamoja nao." Sasa, tunakuwa sehemu ya huo kabla wakati huo haujafika, kutwaliwa katika Unyakuo.

328 Hebu tupeane tu mikono, kwa muda kidogo tu. Ndipo tufumukane, rasmi, kwa dakika moja tu. Tunapoimba *Nampenda*, hebu tupeane tu mikono mmoja kwa mwingine, tuseme, "Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada."

329 "Na . . ." Mungu akubariki. " . . . Yeye." Mungu akubariki, ndugu.

[Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani—Mh.] Wakati wakifumukana, nitafuata, wajua, wasije wakapotelea kwenye umati, mnaelewa.

"Kwani . . ." Mbona, Mungu akubariki, ndugu! . . . ? . . .

> Alinipenda kwanza
> Na kunua wokovu wangu . . .

Mungu akubariki, ndugu.

330 Sasa hebu tuinue tu mikono yetu na kuyafunga macho yetu. Sasa, kwa utamu kabisa.

> Nampenda, na- . . .

Kitendawili SWA64-0418B
(A Paradox)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 18 Aprili, 1964, kwa ajili ya kiamshakinywa cha kimataifa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Cafeteria ya Morrison huko Tampa, Florida, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha Ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na umechapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org